

YEHOVA-YIRE ³



Asante, Ndugu Borders.

Mwaweza kuketi. Ninafanya ushirika tu na Ndugu Harrel, mwenyekiti wa mkutano huu, na kukuta ni mmishenari, nasi kwa namna fulani tuna mambo shirika. Anarudi sasa huko Gold Coast, Afrika. Na mimi ninatarajia kuwa huko mwaka huu. Tulikuwa tukijaribu kuandaa mambo pamoja kuhusu kuitembelea Gold Coast baada ya kutoka Afrika Kusini.

² Ndiko tulikokuwa na, kile ninachowazia, mmoja wa mikutano iliyo mikubwa kabisa, katika siku zangu, ulikuwa ni Afrika Kusini, ambako tuliona wananchi elfu thelathini wanaovaa mablanketi wakimpokea Kristo kwa wakati mmoja. Amina. Waliwaomba wavunje sanamu zao kwenye ardhi, iwapo kweli walimaanisha jambo hilo. Nao wakazivunja sanamu zao, kama dhoruba ya mavumbi inayokuja, na wakamkubali Kristo kama Mwokozi wao, kwenye mkutano mmoja. Walikuwa na mpango mzuri wa kuwafuatilia kule, kwa hiyo waka—wakawapata.

³ Lakini wito mkubwa sana wa madhabahuni ninaoweza kuukumbuka, wa Bwana kutupa sisi, ulikuwa huko . . . ulikuwa huko India, ambako tulikuwa na karibu watu elfu mia tano katika mkutano mmoja. Na kule tu—tusingeweza kabisa kukisia; mbali tu kadiri ungaliweza kuona, ilikuwa ni kila mahali. Na wote hao walimkubali Kristo kama Mwokozi, bali hakuna shirika hata moja la kuwafuatilia. Kwa hiyo basi, bila shaka, Wa—Washiiti waliwachukua wao, Wajaini wakawachukua wao, na kadhalika. Nadhani wengi wao walirudi, baada ya kuona jambo fulani analofanya Bwana na kulileta kule.

⁴ Huduma yangu ambayo Bwana alinipa, katika Marekani haina matokeo mazuri sana, ni Wapentekoste tu. Mengi ya makanisa ya Marekani ni makanisa ya wenye bongo sana, nayo yanaamini kanuni ya imani. Na hapo ndipo tu yanapokaa, huwezi kuwaondoa kutoka hapo.

⁵ Bali wakati unapomchukua mwenyeji na kujaribu kumwambia jambo fulani juu ya kanuni ya imani, hata hajui mkono wa kulia ama wa kushoto ni upi. Itamfaa nini kumpa kitini? Hana budi *kuona* jambo fulani. Na wakati anapoliona, ndipo basi anashawishika. Na anamwona mchawi wake akiinuka na kulipa changamoto, naye anamwona Roho Mtakakatifu analiangusha papo hapo. Naam. Ndipo hilo—hilo linalifunua, kwamba Mungu ni nani, na ndipo hilo linathibitisha.

Na kwa hiyo nina furaha sana kukutana na Ndugu Harrel! Nilikuwa . . . Tulikuwa tukizungumza juu ya wenyenji

wa Afrika. Alikuwa akizungumza juu ya kuufadhili mmoja wa Ndugu T. L. Osborn.

⁶ Wengi wenu mnamjua Ndugu Osborn, nadhani. Loo, huyo hapo mtumishi wa thamani wa Kristo, Ndugu Osborn. Ni mmoja wa marafiki wangu wasiri. Hakika ninamheshimu sana Ndugu Osborn moyoni mwangu, mmishenari mashuhuri kama huyo. Kwa ninii... Ninaamini amefanya mengi zaidi katika huduma ya kimishenari kuliko mtu mwingine yeyote duniani siku hizi, nimjuaye, ni—ni Ndugu Osborn. Mvulana mzuri, mzuri sana, nami bila shaka ninawapenda Ndugu na Dada Osborn.

⁷ Wananiambia ya kwamba Mama Arganbright yuko mkutanoni usiku wa leo. Je! unajificha kutoka kwangu, Mama Arganbright? Hakika ninathamini tunda lako zuri. Na si ajabu yeye ni mama mdogo mzuri jinsi hiyo, ametokea sehemu hii ya nchi hapa. Daima anazungumza juu ya Grass Valley. Ni wangapi wanaomjua Bw. na Bibi Arganbright, kwenye maeneo ya Grass Valley? Vema, hilo ni jambo zuri. Uko wapi, Mama Arganbright? Sijakuona kwa muda mrefu sana, ulichurupuka... Yule pale. Naam. Namtakia heri. Nyumba yake ni makazi yangu ya pili, mwanamke mzuri sana papa hapa kutoka Grass Valley. Naye daima amekuwa na mzigo wa watu hawa. Na Mama Arganbright, kama huu ndio usiku wako wa kwanza hapa, nilikuwa huko mwituni nikiomba leo wakati ulipomtembelea mke wangu na hao wengine. Nami nasikitika sikuwako nipate kukuona, na kukutana na rafiki yako.

⁸ Lakini nitasema ya kwamba nimeona jambo fulani likitukia miongoni mwa watu wenu hapa ambalo sijalion katika jiji lolote la Marekani popote. Nimeona Wakristo wakitambua ya kwamba wamekosea, katika Neno la Mungu, na kusimama na kuomba rehema. Naam. Hilo linasikika kwangu kana kwamba uamsho ungeweza kuibuka hapa. Lingekuwa ni jambo zuri sana. Ingawa nimehubiri kote ulimwenguni, na hasa sana Marekani, sijapata kuona kabla ya hapo, makundi ya Wakristo, wakati Neno lilipohubiriwa, kulifunua Neno, watu walisimama na kusema (wakashuhudia) walikuwa wamekosea. Si hivyo tu, bali wahudumu pamoja nao. Sasa, huo ni uaminifu. Ninapenda jambo hilo.

⁹ Dada Arganbright, kwa kuwa walikufanya usimame, nitamtahayarisha mke wangu. Yeye ndiye mtu mwenye haya kuliko wote ulimwenguni. Hata hivyo ameketi hapa usiku wa leo. Mpenzi, ninaamini utajilipizia kisasi kwangu kwa ajili ya jambo hili, bali nitamwomba mke wangu asimame. Mwanamke mzuri kuliko wote ulimwenguni, kwangu mimi. [Kusanyiko linashangilia—Mh.]

¹⁰ Msichana wangu, binti yangu, binti yangu mkubwa, Rebekah. Sasa, kipenzi, ninajua umechomwa na jua, bali ninakutaka usimame, haidhuru. Vema, Rebekah. Huyu ni binti

yangu, Rebekah. [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Asanteni. Asanteni.

¹¹ Ndugu Jewel Rose, ni wangapi wanaomfahamu? Usiku mmoja alimfanya mke wangu kuja jukwaani nilipokuwa, baada ya ibada kuanza. Karibu azimie. Yeye humkwepa tu popote anapoweza kumwona. Yeye humwepuka, kwa sababu anaogopa atamwita jukwaani tena.

¹² Nilimwambia, “Usiku mmoja nitakufanya usimame na kutuzungumzia kidogo.”

¹³ Akasema, “Iweke ndoo ya maji tayari, kwa sababu nitazimia.”

¹⁴ Yeye ni mtu mpendwa sana, mke wangu. Kama kuna sifa yoyote ya kupewa familia ya Branham, acha imwendee yeye. Yeye ndiye aliyesimama kati yangu na umma. Na mambo yote ambayo yamefanywa vizuri, yeye ndiye ameyafanya.

¹⁵ Ninatumaini ya kwamba kila kijana mwanamume hapa, wakati atakapooa, atapata mke, nanyi mtaishi mkiwa na furaha pamoja kama vile mimi na mke wangu tumefanya miaka hii ishirini na miwili ambayo tumefunga ndoa.

¹⁶ “Yeye aliyempata mke, amepata kitu kizuri.” Kama alivyosema Sulemani, “Mwanamke mzuri ni johari kwenye taji ya mwanamume. Asiye haki ni maji damuni mwake.” Na mzunguko wake wa damu ni maisha yake. Kwa hiyo, mwanamke mwovu ni kitu kibaya zaidi anachoweza kupata. Na mwanamke mwema ni kitu kizuri sana anachoweza kupata, nje ya wokovu. Kama Mungu angaliweza kumpa mtu kitu kizuri zaidi kuliko mke, angalimpa, maana Mungu huwapa tu watoto Wake vitu vizuri. Naye alimpa mke, nami ninashukuru kwa ajili ya jambo hilo.

¹⁷ Na kuwaona wanawake, wakati kwa namna fulani nilikuwa nikiwakatakata hivi majuzi usiku, kwa Maandiko juu ya vile hawa wanawake wa Kipentekoste wanavyovaa, wanavyoweka nywele zao, na kuendelea hivyo na maisha. Mnasema, “Hilo halileti tofauti yoyote.” Hakika linaleta tofauti!

¹⁸ Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Ndugu Harrel yupo hapa, mmishenari.

¹⁹ Huko Durban, Afrika Kusini, wanawake walikuwa wameketi kule wakiwa uchi jinsi walivyokuja duniani; kamwe hawakuwa na nguo hata moja, ni kipande tu kidogo, cha kama inchi nne, sita mbele zao. Nao wamesimama pale uchi tu kadiri walivyokuwa, nao wakiwa wamesimama kule uwanjani baada ya mwujiza huu mkuu kufanyika jukwaani. Na katika kundi hilo kulikuwa, lilikuwa na karibu Waislamu elfu kumi (wakati mmoja) waliomkubali Kristo kwenye mkutano uo huo. Halafu mle ndani wakati... Wanawake hawa, wakisimama pamoja na hawa wanaume, walimkubali Kristo.

20 Ndipo Ndugu Bosworth akasema, “Ndugu Branham, ninaamini unapaswa kufanya wito huo tena. Ninaamini walimaanisha uponyaji wa ‘kimwili.’”

21 Nikasema, hakika, wakalimani kumi na watano mbalimbali. Unajua, inahitaji... Inakubidi tu kuandika kile umesema, ifikiapo wakati wao... Unasema, “Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, alikuja kuwaokoa wenye dhambi.” Na huyu atasema “blu, blu, blu, blu,” na huyu atasema, “nic, nic, nic, nic,” hayo ni “Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.”

22 Mnajua, ni—nilikuwa nikiwasikiliza watu wakinena kwa lugha, nami nikawazia, “Jamani, hilo haliwezi kuwa ni sahihi.” Lakini Biblia ilisema, “Hakuna sauti isiyo na maana.” Hakuna. Niliposikia jambo hilo, wengine wao hupiga kidoko kama ndege, wengine wana kilio chembamba kama cha wadudu, na kila kitu. Lakini inamaanisha maana fulani kwao, kama kila sauti ilikuwa na maana.

23 Na wakati ulipotolewa tena, nami nikasema, “Vema, basi hebu wale ambao kweli wanajua ya kwamba si uponyaji wa ‘kimwili,’ ni kumkubali Kristo kama Mwokozi, Mbingu wa kuendea, unamwamini Mwana wa Mungu, unamkubali kama Mwokozi wako binafsi, vunjilieni mbali sanamu zenu ardhini!” Nao wakazitupa chini. Ndipo nikasema, “Papo hapo sasa, mwinulie Mungu huyo mikono yako, na umpe sifa. Yeye atakupua Roho Mtakatifu!”

24 Na wakati nikisimama katika uwanja ule, niliwaona wanawake waliokuwa uchi wa mnyama; na mara Kristo alipowagusa, waliondoka mahali hapo huku wamekunja mikono yao. Na wakati ulipowaona tena, walikuwa wamevaa nguo.

25 Sasa, kama Kristo atamfanya kafiri (aliye uchi) atambue kwamba amekosea, kwa kuwa uchi, halafu wanawake wanaodai kuwa ni Wakristo na kila mwaka wanavua nguo zaidi, siwezi kuelewa hilo. Kuna kasoro mahali fulani.

26 Kafiri kwelikweli, akiwa tu amesimama pale, amezaliwa humu ulimwenguni na kamwe hakujua alikuwa uchi, hajui yu uchi. Lakini hebu acha Kristo aje mbele zake, yeye anatambua yu uchi, hata anajaribu kujifunika vizuri kadiri awezavyo, kukunja mikono yake na kuondoka. Siku mbili ama tatu baadaye, utamwona tena, amevaa nguo.

27 Sasa kuna kasoro fulani mahali fulani, nami nina hakika si na Kristo. Loo, ninafikiri Neno ni kamilifu!

28 Ninaipenda sana safari ya Ibrahimu. Nanyi je? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ninakaa nayo muda mrefu sana, ninatumaini nitafikia *Yehova-Yire* usiku wa leo. Nililichukua somo hili, siku tatu ama nne usiku zilizopita, wala kamwe sikulifikia.

²⁹ Lakini mwaka mmoja huko nyumbani nilichukua somo, nikihubiri juu ya Ayubu. Vema, karibu mwaka mmoja nilikuwa kwenye Kitabu cha Ayubu, kila Jumapili na Jumatano, juu ya Ayubu. Ndipo hatimaye nikampandisha juu hata akaketi kwenye lundo la majivu. Nilimweka pale karibu majuma matatu ama manne. Ndipo dada mmoja—mmoja wa thamani mwenye ujasiri wa kutosha kuniandikia, alisema, “Ndugu Branham, utamtoa Ayubu lini kwenye lundo hilo la majivu?”

³⁰ Vema, nadhani mnashangaa ni wakati gani nitakapompandisha Ibrahimu akamwone Yehova-Yire.

³¹ Lakini nilikuwa na jambo muhimu. Ibrahimu. . . Au, Ayubu akiketi pale kwenye lundo la majivu, Elihu akinena: Mungu akimjaribu mtakatifu. Nikayaingiza yote ndani, mpaka nikafika mahali ambapo ningeweza kutupa risasi ya kuua, nikaandaa kila kitu. Ndipo Bwana akashuka katika upepo huu wa kisulisuli, na umeme ukaanza kumulika, na ngurumo kunguruma. Ndipo Roho wa Mungu akamjia nabii huyo, akasimama kwa miguu yake, akasema, “Ninajua kwamba Mkombozi wangu yu hai,” angalia “Mkombozi.” “Na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi. Na ingawa baada ya mabuu ya ngozi kuuharibu mwili huu, bado nikiwa na mwili wangu nitamwona Mungu; ambaye nitamwona kwa nafsi yangu, macho yangu yatamwona, na wala si mwingine.” Loo, ni somo la jinsi gani pale! Kulishindilia hilo ndani, ilichukua muda mrefu kuwaweka watu tayari kabisa, Roho ikiwa sawa, kisha kulishindilia. Ndipo madhabahu ilizungukwa na kujazwa na watu, wakitubu.

³² Kama tu unaongozwa na Roho, chukua tu wakati wako mpaka utakapolenga shabaha kwelikweli. Usipolenga, utapiga risasi juu zaidi ama uipige mbali sana, ama kitu kama hicho. Hebu na tulenge kikamilifu, Biblia! Ninaamini ya kwamba Mungu anatutaka tulenge kikamilifu. Roho Mtakatifu aliilenga kikamilifu kwa mitume, ama wao walikuwa wameilenga kikamilifu kwa Roho Mtakatifu, hasa. Nami ninaamini tunaweza kufanya jambo lile lile, kwa Neno lile lile. Ni kulenga shabaha! Na kama lililenga mara moja, katikakati kabisa, linaweza kuilenga tena! Lakini inakubidi kuilenga kikamilifu! Uwe na hakika kupumua kwako, kuvuta kwako, kila kitu ni sawa tu kabisa. Mimi hulenga shabaha; ninajua ni kitu gani, ni kulala kwenye mashindano, na bunduki itakayolenga shabaha.

³³ Wakati mmoja niliirudisha maskini muundo wa sabini na tano kwa Kampuni ya Winchester, siku moja. Nami nisingeweza kuifanya ilenge karibu ninii tatu. . . ama robo inchi, umbali wa yadi hamsini. Ndipo kampuni ya Winchester ikairudisha kwangu, wakasema, “Kasisi Branham, bunduki hiyo imetengenezwa tu ku—kurusha lundo la risasi tano, inchi moja kwenye umbali wa yadi ishirini na tano.” Sasa hiyo ilikuwa ni kampuni iliyoitengeneza. Ninajua tofauti. Nilirusha, moja baada ya nyingine, kwa usahihi, vishikizo tisa vya zulia, moja

kwa moja, kwenye umbali wa yadi hamsini, nayo. Kwa hiyo nilijua ilikuwa imelengwa kikamilifu. Kwa hiyo nikaendelea tu kuijaribu, na kuijaribu, mpaka nikaifanya ilenge tena.

³⁴ Sasa, ni jambo lile lile kwa Neno la Mungu. Hayo mambo hao mitume waliyofanya, hayo mambo ambayo Kristo aliahidi, hatuna budi kuyalenga kwa Neno, kwa Roho. Kama lilifanya jambo hilo wakati mmoja, litalifanya tena, kwa maana ni Mungu. Naye Mungu ni Neno, wala hawezi kushindwa.

³⁵ Kama kuna kizuizi fulani, bunduki ikiwa imelegea sana *hivi* kwenye mkono wa mbele, imelegea kidogo ama imekazwa sana, chochote kinachoikaza, unaweza kuweka uzito wa kidole chako kwenye bunduki, na (ikilenga kikamilifu) uzito wa kidole chako utaitupilia mbali. Huna budi kuwa na kila kitu kikamilifu.

³⁶ Hivyo ndivyo inavyokubidi kufanya katika Ukristo, kulifanya Neno, kulifanya lidhihirike na kufanya ipasavyo, wewe mwenyewe pamoja na Neno na pamoja na Mungu, haina budi kuwa ni jambo kamilifu, ndipo basi litalenga kikamilifu. Haina budi kufanya hivyo! Kwa hiyo basi, katika kuhubiri, huna budi kumhisi Roho Mtakatifu sawasawa kabisa, kisha ulenge kikamilifu; hiyoo itaenda, italenga shabaha.

³⁷ Halafu watu wanaoketi karibu, mara nyingi watu husema, “Ndugu Branham, sisikii habari za mikutano yako.”

³⁸ Sina njia za matangazo kama walizo nazo hao ndugu wengine. Wana magazeti, wana—wana radio, televisheni. Mimi ninapita tu nikijaribu kumwakilisha Bwana Yesu. Watu wanaliona, wanaliadini, wanapona. Mungu anajua hayo, hilo tu ndilo muhimu. Unaona? Hatuninii, sisi si... Hakutakuwako na historia yoyote itakayoandikwa. Usijali juu ya jambo hilo. Hakutakuwako na wakati wa kuiandika historia. Ninaadini Yesu anakuja. Hilo, ninaliadini. Nami ninataka kuishi leo kana kwamba Yeye angekuja leo hii ama kesho. Sio shule kubwa mashuhuri, na kadhalika. Mbona tunafanya mambo hayo, halafu tunahubiri Yesu yuaja? Mbona, kazi zetu wenyewe zinashuhudia dhidi yetu. Hiyo ni kweli. Yesu yuaja, hebu tuninii, tulifanye kanisa liwe tayari kwa ajili yake! Hebu na tuwe tayari. Loo, jinsi ninavyompenda!

³⁹ Na tunamishe vichwa vyetu sasa kwa maombi. Loo, jinsi ninavyompenda kuwaona watu wakati wanapoinamisha vichwa vyao kwa kicho. Sasa hebu na tukae kimya kwa muda kidogo, na kusoma. Sasa tunataka kuchukua wakati wetu. Kesho ni Jumapili, sabato, siku ya sabato ya Wakristo. Nami sitaki mchelewe kwenye shule ya Jumapili, ingawa hatutaki kuyaharakisha mambo haya.

⁴⁰ Wazieni sasa, “Bwana, je! shauku ya moyo wangu usiku wa leo inalingana na mapenzi Yako?” Kama ndivyo, basi wewe iwazie. Ndipo kama ukiiwazia, haja yako, na kuichunguza kwa mpango wa Mungu. Kama ikionekana inaambatana vizuri

na mpango wa Mungu, basi ninakutaka uinue mkono wako kwa Mungu, na kusema, “Mungu, nikumbuke, hii ndiyo haja yangu.” Wazia tu kwa makini sana. Mungu akubariki. Vema. Bwana akubariki. Hilo ni zuri. Endelea tu kuinua mkono wako. Yeye anaona yote. Anajua mambo yote. Hilo ni zuri. Mungu akubariki. Amina. Bwana akubariki. Hilo ni zuri. Endelea tu kuwazia, ukiinua mkono wako. Sasa ninauangalia kila mkono unapoinuliwa. Vema. Hilo ni sawa.

⁴¹ Baba wa Mbinguni, tunakuja sasa, tukikaribia tena katika Jina hilo linalotosheleza katika yote la Bwana Yesu, mpaka kwenye Kiti cha Enzi cha Rehema. Kama vile mshairi alivyosema, “Nijalie nikiwa kwenye Kiti Chako cha Enzi cha Rehema, nipate uhuru mtamu.” Na, Mungu, mioyo yao imelemewa na jambo fulani. Basi wajalie sasa, hapo kwenye Kiti cha Enzi cha Rehema, wapate faraja ambayo Mungu anawamiminia, yule Tabibu mkuu, na imani kwa ajili ya yale wanayohitaji.

⁴² Nimeinua mikono yangu miwili. Nina haja nyingi. Nikumbuke, Bwana.

⁴³ Wakumbuke watu hawa wote hapa ambao wanawakilishwa na lesi hizi. Loo, jinsi ambavyo shuhuda zimeingia kwa ajili ya mambo haya. Uchaji. Huko mbali ng'ambo ya vilima hivi vya mchanga hapa, mahali fulani, mama wagonjwa, baba, watoto wachanga, watu walio hospitalini, maskini baba mkongwe kipofu akiwa ameketi huko nyuma kwenye chumba kidogo akiwa na fimbo nyeupe mkononi mwake, akingojea kurudishwa kwa lesi hizi. Mungu, turehemu. Tujalie, Bwana, ya kwamba yeyote ambaye zitawekwa juu yake, adui na apoteze uwezo wake na nguvu, jalia waende na wakaponywe. Hii hapa moja imeandikwa hapa, “kansa.” Jalia ibilisi huyo awaachilie, Bwana. Jalia Roho Mtakatifu, wakati Mungu akiangalia chini kupitia kwenye Damu ya Mwanawe aliyekufa kwa kusudi hili, jalia ule upatanisho mkuu utosheleze usiku wa leo, na imani iwe inabubujika kwa wingi juu yao, na jalia...ama kwa wingi, wapate kuupokea uponyaji wao. Lijalie, Bwana.

⁴⁴ Libariki Neno Lako sasa. Msaidie mtumishi Wako, tutie mafuta kwa ajili ya ibada hii. Utie mafuta kila moyo unaosikiliza. Nasi tutazungumza tu sasa, Baba. Naomba utwambie la kusema, na utwambie la kufanya. Tunakutarajia Wewe uwe pamoja nasi mkutanoni.

⁴⁵ Asanteni kwa nyimbo nzuri usiku wa leo, hizo nyimbo nzuri za dini. Huyu kijana mwanamume hapa nyuma, Ndugu Heimer, ndiyo kwanza aimbe wimbo ule mzuri sana wa dini, *Yule Mgalilaya*. Jalia yule Mgeni wa Galilaya aingie sasa usiku wa leo. Jalia tuisikie sauti Yake ikiuambia moyo unaosumbuka, kama alivyoyafanyia yale maji yaliyotibuka, “Amani, tulia.” Na

jalia kila moyo unaosumbuka uponywe. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Naye akapaita mahali pale Yehova-Yire, kama ilivyoandikwa hata leo, katika mlima wa BWANA itapatikana.

⁴⁶ Sasa tunataka kuanza na mtu huyu mashuhuri. Na kesho... Sasa, Bwana akipenda, tutajitahidi kufikia mwisho kumhusu Ibrahimu usiku wa leo. Na kesho, labda fungu la maneno juu ya uponyaji wa Kiungu.

⁴⁷ Bwana amekuwa mwema kwetu hapa. Tumekuwa tukisikia shuhuda za mambo yaliyotukia. Nasi tuna furaha sana! Nasi tulikuwa na usiku mmoja, mstari mzima wa maombi, ama kuwaita. Wala hapakuwapo na mtu mnyonge tuliyemwona humu jengoni, kiti cha magurudumu, popote, ila wale waliokuwa wamesimama, wakitembea-tembea, wakienda.

⁴⁸ Na sasa kila usiku Roho Mtakatifu amekuja katika Uwepo Wake adhimu na mtukufu sana, na amewaendea wasikilizaji, akijitangaza Mwenyewe, ya kwamba Yeye yupo hapa. Kwa hiyo, inatupasa kumwamini. Unaona, Yeye anawataka ninyi mmwamini. Heshima kubwa sana unayoweza kumpa Mungu ni kumwamini Yeye. Huna budi kuamini. "Yeye amjiaye Mungu hana budi kuamini ya kwamba Yeye yuko." Na sasa mwamini Yeye!

⁴⁹ Na ninapomchukua Ibrahimu, ile safari, ni kwa sababu tu ninajaribu kuijenga imani kwa ajili ya kipeo kikubwa, kuwafanya watu waone kwamba wao ni akina nani.

⁵⁰ Hiyo ndiyo shida. Ninakuta matabaka mawili ya watu, ninaposafiri. Moja la hayo ni la kipentekoste, hilo jingine ni la kimsingi. Sasa, wa kimsingi wanajua mahali walipo, kwamba wao ni akina nani, bali hawana imani yoyote na jambo hilo. Mpentekoste ana imani, bali hawajui kwamba wao ni akina nani. Sasa, ni kama tu mtu aliye na fedha kwenye benki, bali hajui jinsi ya kuandika cheki; na huyo mwingine anaweza kuandika cheki, na hana pesa kwenye benki. Laiti ungaliweza tu kuwaweka pamoja, jambo fulani lingetukia. Ukiwahi kupata imani ya kipentekoste na fundisho la kimsingi, kama ungeweza...ama labda upate fundisho la kimsingi na imani ya kipentekoste, jambo fulani litatukia. Hiyo ni kweli.

⁵¹ Sasa, jinsi ambavyo ningetaka kutoa ushuhuda hapa, wakati nilipoona, shule ya Kilutheri, watu mia nne wakiupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu wakati nilipokuwa nikiongea nao juu ya jambo hilo. Loo, jamani, lilikuwa ni tamasha la ajabu, kuwafanya wajue jambo hilo. Wao hawajaninii, maana wao ni Walutheri, hawajawekwa nje.

⁵² Hakuna kitu dhidi ya Mlutheri, Mbaptisti, Mmethodisti, chochote ulicho, Mkatoliki. Mimi sivipingi vitu hivyo. Siwapingi watu hao. Ni ule mfumo unaowashikilia, ndio ninaonena dhidi

yake. Sina neno dhidi ya mtu binafsi, wote ni wanadamu ambao Kristo aliwafia; Mkatoliki, Myahudi, chochote alichu. Ni huo mfumo. Kama vile Mwislamu, Mshiite, Mjeini, ama yeyote yule, ni huo mfumo. Mbuddha ni mfumo, unaona. Sio hao watu ambao—ambao wanamwabudu Buddha; ni huo mfumo unaowavuta kuwaondoa kwake.

⁵³ Hilo ni jambo lile lile. Yesu hakuwapinga watu hao. Yeye aliwafia. Bali hiyo mifumo iliyokuwa ikimzuia, ikiwazuia wasimkaribie. Jambo ndilo hilo sasa.

⁵⁴ Sasa niliwazia, katika kumchukua Ibrahimu, tukijua ya kwamba ahadi ilitolewa kwa Ibrahimu, na Uzao wa Ibrahimu baada yake. Sasa hebu tusafiri nyuma kidogo na tupate msingi wake, ndipo tuje usiku wa leo moja kwa moja kwenye somo sasa kwa muda kidogo.

⁵⁵ Na kadi za maombi zitatolewa kwa mtu yeyote anayetaka kuombewa. Nasi, kama hamuwafikii wote usiku wa leo, tutawafikia kesho. Na mtu yeyote anayetaka kuombewa hana budi kuwa na kadi ya maombi. Na awe hapa saa saba na nusu kesho, kuchukua kadi yako ya maombi, kwa sababu tunataka kuanza mkutano wakati huo. Na tutamwombea kila mtu aliye na kadi ya maombi kesho. Tumekuwa tukijaribu, usiku kucha, kuwapata wale wasio na kadi za maombi, ili kwamba wale walio na kadi za maombi watakuwa na majaliwa ya kuwa kwenye mstari wa maombi. Na wengine wanaitwa kule, bila kadi za maombi. Hiyo inawapata wote wawili, pande zote mbili. Kadi ya maombi haina maana yoyote. Lakini unapompa mtu kadi ya maombi, kuna kama asilimia arobaini wanaoponywa papo hapo, ni wewe kuwazia anapitia mstarini; kitu fulani anachoweza kushikilia, kitu fulani anachoweza kukitazama, ama chochote kile. Basi m—mvulana atakuwa akisambaza kadi za maombi kesho kwenye saa saba na nusu, kusudi waweze kutoka ifikapo saa nane, kwa hiyo ra—ratiba yote ya siku iliyosalia wataipata.

⁵⁶ Nanyi mnaotaka picha, kitabu, ama kanda, hamna budi kuvipata usiku wa leo. Hakuna kuuza Jumapili; kamwe haturuhusu jambo hilo, kuviuza. Tunaiheshimu Jumapili, kamwe hatuuzi Jumapili. Na vitabu hivi na kadhalika, hivyo si kitu kwangu, hivyo ni vitabu ambavyo watu wameandika kuhusu huduma yangu. Picha ambazo Shirika la Marekani la Wapiga Picha waliipiga picha hiyo, na ni mali ya Douglas Studio, imehatimilikiwa. Hicho kitabu ni cha Ndugu Gordon Lindsay na Kasisi Julius Stadskev. Sisi huvinunua na kuvileta mkutanoni, nasi tunaviuza karibu na vile tunavyovipata, na tunapata hasara kwake. Nasi daima tulisema jambo hili, kama yeyote. . . Nimewaambia watu wanaoviuza vitabu, “Kama mwanamume ama mwanamke akija pale, maskini, hana pesa za kukinunua kitabu hicho; wapeni, haidhuru. Nasi tutaninii. . . Nitahakikisha limeshughulikiwa.” Na endapo una kitabu hicho wala hakifai kwa bei hiyo, kirudishe. Kamwe hakutakuwako na

mtu atakayekirudisha pasipo kurudishiwa pesa zako, unaona. Ni kitu fulani tu cha kuisaidia imani yako. Hiyo tu ndiyo sababu ya sisi kufanya hivyo, la sivyo tusingeruhusu jambo hilo hapa. Hiyo ni kweli kabisa. Kwa hiyo sasa usiku wa leo, kumbukeni, watakuwa kwenye kituo cha vitabu. Rafiki msiri wangu, Bw. na Bibi Wood. Laiti ningalikuwa na wakati wa kuwaambia ushuhuda wao, jinsi ambavyo mvulana wao alivyoponywa polio. Na mambo mengine mengi yame—yametukia, ya watu walio hapa mkutanoni.

⁵⁷ Sasa hebu na tumwekee Ibrahimu msingi. Kwanza, Mungu alikutana na Ibrahimu, bila masharti, agano alilofanya na Ibrahimu. Hakuna kitu hata kidogo; Ibrahimu hakuwa na la kufanya ila kumwamini Mungu. Hilo agano lilikuwa ni kwa neema tupu, na lisilo na masharti. Sio “kama ukifanya.” Mungu alisema, “Nimefanya!” Na sasa kila mtu. . .

⁵⁸ Kumbukeni, Uzao wote wa Ibrahimu unaopata kumjia Mungu, unamjia vivyo hivyo. Sio jambo fulani ungaliweza kufanya! Usingeweza kujiokoa kadirini usivyoweza kukamata kamba ya viatu vyako na kuruka juu ya mwezi. Huwezi kujiokoa. Hakuna mtu aliyepata kumtafuta Mungu; ni Mungu anayemtafuta mwanadamu. “Kamwe hamkunichagua Mimi,” Yesu alisema, “Niliwachagua.”

⁵⁹ La kwanza, sasa, je! ungaliweza kutoka kwenda huku na kumwambia nguruwe kwamba amekosea, akila takataka? Atakwambia ushike lako. Lakini itabidi kuchukua kitu fulani kitakachoibadilisha tabia yake, kumfanya atambue ya kwamba amekosea. Jambo fulani halina budi kutukia kwa nguruwe huyo, kwanza.

⁶⁰ Hiyo ndiyo sababu wanaodhaniwa ati ni Wakristo mara nyingi hugaagaaa matopeni, wanarudi dhambini, ni kwa sababu. . . Ungaliweza kumwosha nguruwe, na kupaka makucha yao rangi, uwapake rangi midomoni. Hilo, hilo ni kosa, chochote kile. Rangi ya mdomo, sivyo, ama chochote kile? Ninachanganya, hilo, takataka hizo zote. Mnajua ni kitu gani, haidhuru. Wewe mpake maskini nguruwe huyo jike rangi ya mdomo na—na, unajua, umshughulikie na mengine yote, naye ataenda moja kwa moja kwenye matope, na kugaagaa tena. Kwa nini? Kwanza kabisa, yeye ni nguruwe. Jinsi tu utakavyomfanya tofauti, ni kubadilisha asili yake.

⁶¹ Hivyo ndivyo tu mwanamume ama mwanamke anavyoweza kupatana na Mungu, ni kubadilisha tabia, kujisafisha, kufia dhambi ya yule mtu wa kale, na kuzaliwa tena kwa Roho wa Mungu. Na, hiyo ni kusema, Kristo ni Roho wa Mungu, na Kristo ni Neno. Basi anashuhudia pamoja na Neno. Hivyo ndivyo tu watakavyoweza kufanya jambo hilo.

⁶² Sasa, Ibrahimu alikuwa akiutafuta Mji Ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni ni Mungu. Na leo hii sisi ni wasafiri,

wageni, tukiutafuta Mji ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni ni Mungu. Angalia! Ibrahimu, kabla hajapata kujua, kulikuwa na kitu kama silika ndani yake, kwamba aliutafuta huo Mji.

63 Leo, nikipita pamoja na mke wangu, nilikuwa nikisema, “Mji mdogo unaopendeza huu hapa juu ya mlima, labda miaka mia tatu iliyopita; msitu mzuri, miti mikubwa mirefu. Mwanadamu akaingia, wakaikata, wakavichafua vijito. Pangekuwa ni mahali pazuri pa kuishi hapa.” Naam, lakini ukiangalia, yeye alijenga nyumba. Kisha wakaanza kuongezeka. Dhambi na vurugu zikaanza kuingia. Hollywood ikaja karibu naye, ikiletwa na sinema, na televisheni. Kwa... Na sasa pameambukizwa, pamejaa dhambi, kila mji!

64 Na hakika, kama watu, kitu fulani ndani yao hupenda waishi pamoja, kuwa na jirani, na wawe wenye haki. Hakika kuna Mji mahali fulani! Kilindi kikiita Kilindi tena!

65 Naye Ibrahimu aliiona miji ya siku zake, Uru wa Wakaldayo. Naye alijua hilo kwa sababu kulikuwa na kitu fulani ndani yake kikiita, kulikuwako na Mji uliokuwa tofauti, ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni alikuwa ni Mungu. Naye Mungu akaona jambo hilo ndani ya Ibrahimu, akamwambia, “Jitenge sasa, utoke humo.”

66 Sasa, Ibrahimu, jambo moja ninalotaka mwone, alitii Neno la Mungu kikamilifu.

67 Daima kumbukeni jambo hilo! Huo ndio Ujumbe wangu. Hamna budi kutii Neno. Na ukijua chochote kinyume na Hilo, kiache. Huenda kikaonekana ni kizuri, bali usitoe hoja dhidi ya Neno la Mungu.

68 Hilo ndilo jambo la kwanza Shetani alilofanya, ilikuwa ni kutoa hoja dhidi ya Neno la Mungu, kwa Hawa. Wala mwanamke hakulishuku. Alilihoji tu. Shetani alilihoji.

69 Na hivyo ndivyo wanavyofanya siku hizi. “Je! si ni jambo la maana kwamba tunapaswa kufanya jambo *hili*? Si ni jambo la maana?” Kama liko kinyume na Neno la Mungu, liache! Ni Sauti ya Shetani.

70 Liruhusu Neno, kama Neno limo ndani yenu... “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, basi ombeni mtakalo.” Roho Mtakatifu! “Mkikaa ndani Yangu, Neno Langu ndani yenu,” hilo ni Neno lililofanyika mwili, “ombeni mtakalo nalo litatimizwa.” Hiyo ndiyo njia. Ondoeni kanuni zote za imani, vitu vyote mbali, kisha mlishikilie Neno kwa maana ni Kristo. Angalieni, ndipo litajidhihirisha lenyewe.

71 Mtu fulani alisema, “Ndugu Branham, unajua mambo hayo. Unajua?”

72 Haya unayoyaona hapa mkutanoni ni mambo madogo. Mtu yeyote hapa anayesafiri pamoja na mikutano, anajua. Roho Mtakatifu huyafunua mambo ambayo huja majuma na

miezi katikati ya wakati. Na hebu mwulize mtu yeyote, “Je! limewahi kukosea hata wakati mmoja?” Haliwezi kukosea, unaona. “Unajuaje hilo?” Kwa sababu ni ahadi ya Neno, na wakati umewadia. Halina budi kutimia. Sasa, sijui, kutakuwako na wachache sana, walio wachache wataliamini, bali halina budi kutangazwa haidhuru. Na uliwahi kuona, linapita moja kwa moja juu ya kichwa cha watu, na linapita na kutoweka kabla hawajalitambua. Daima namna hiyo.

⁷³ Kweni ninyi Wakatoliki, mnajua vile kanisa leni lilivyofanya? Kwa sababu Joan wa Arc alikuwa ni mtakatifu ha—halisi wa Mungu, alifanya miujiza ya Mungu, akatabiri mambo ya Mungu. Nanyi mkamwita mchawi, na kumchoma kwenye nguzo; naye akilia apate rehema, nanyi mkamchoma kwenye nguzo. Mamia ya miaka baadaye, mkatambua mlukosea, ndipo mkamfanya mtakatifu. Alipita moja kwa moja juu yenu, wala hamkumjua.

Elia alipita, hawakumjua. “Mzee bingwatapeli!”

⁷⁴ Kristo alipita, hawakumjua baada ya kufa, kuzikwa, na kufufuka Kwake. Mungu huweka jambo hilo. Nalo linamchenga kabisa asiyeamini. Na kuonyesha... Yeye alisema, “Nimeyaficha kwa macho ya wenye hekima na akili, na kuwafunulia watoto wachanga ambao watajifunza.” Kristo alimshukuru Mungu kwa kufanya jambo hilo. Unaona?

Jinyenyekeze. Liimini. Lijaribu Neno.

⁷⁵ Yesu alisema, “Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani yake mnafikiri mna Uzima wa Milele, nayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Mlipaswa kuijua ile saa.” Kasema, kawaambia Mafarisayo, “Enyi wanafiki, mnaweza kuutambua uso wa mbingu. Bali ishara za wakati, hamwezi kuzitambua. Kwa kuwa kama mngalinijua Mimi, mngalijua siku Yangu.” Akapita moja kwa moja juu yao, hawakujua jambo hilo mpaka lilipokuwa limepita. Angalieni sasa Neno likiwa ni muhimu sana!

⁷⁶ Hebu angalieni lingine, wakati tukiwa kwenye hilo, Lutu. Yesu alisema, Mwenyewe, “Kumbukeni mke wa Lutu.” Kama Neno si muhimu sana, kama kutoa hoja ni sawa; wakati Malaika huyo alipomwambia Lutu na familia yake, “Nenda Soari, bali usiangalie nyuma!” Na mke wa Lutu, kwa jambo dogo lisilo na maana la kugeuka na kuangalia nyuma, bali lilikuwa ni kinyume na Neno, aligeuka akawa nguzo ya chumvi.

⁷⁷ Halafu unasema, “Kuwaambia wanawake juu ya kukata nywele zao, kuvaa nguo...?” Mungu alisema usifanye hivyo! Wewe lifuate Neno. Lutu alikuwa na, hapana shaka, mke mzuri, bali hakuitii Amri ya Neno. Lutu! Hawa alikuwa mwanamke mzuri, bali hakuifuata Amri ya Neno; alilitolea hoja kidogo tu.

⁷⁸ “Hivi si ni jambo la maana, Ndugu Branham, ya kwamba inatupasa kufanya jambo hili? Mimi ni mwenyeji wa Marekani,

ni—nina haki ya kufanya lolote nitakalo. Hiyo ni haki yangu ya Kimarekani.” Ni haki yako ya Kimarekani, bali si haki yako ya Kikristo. Kwa maana, ukiwa ni Mkristo, wewe ni mwana-kondoo; na kondoo huachilia haki zake. Yeye hulala kimya na kukuacha umnyang’anye haki zote alizo nazo. Bali mbuzi atafanya vurugu kubwa kuhusu hilo. Hiyo ni kweli. Bali mwana-kondoo huachilia haki zake. Na Mkristo daima huachilia haki zao za kitaifa kama zinapingana na haki zako za Kikristo.

⁷⁹ Mke wa Lutu aliangalia tu nyuma, [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] basi! Sasa hilo lilifanya nini? Linatwambia hapa katika Ibrahimu, na Lutu, ya kwamba jambo waliloweka pale, mfano. Nasi hatuwezi kulikwepa.

⁸⁰ Waebrania, mlango wa 11, ilisema, “Mambo haya yalikuwa ni mifano kwetu. Kwa kuwa tumezungukwa na wingu kubwa sana la mashahidi. Tunapaswa kuweka kando kila dhambi.” Dhambi ni nini? Kutokuamini! “Kila dhambi, kila kutokuliamini Neno la Mungu, kunakotuzinga kwa upesi.”

⁸¹ Tunapokabiliwa na jambo fulani, anasema, “Vema, wanahubiri jambo *hilo*, ya kwamba *hilo* lilikuwa . . .” Msifanye hivyo! Fanyeni tu yale Mungu aliyosema mfanye. Dumuni nalo, kikamilifu!

Unasema, “Haileti tofauti yoyote.”

⁸² Vema, jambo pekee ninaloweza kusema ni lile Neno linalosema. Na Yesu alitilia hilo mkazo, “Mkumbukeni mkewe Lutu.” Aliangalia tu juu ya bega lake. Hawa alisimama tu kwa muda kidogo. Hivyo tu ndivyo alivyofanya. Mke wa Lutu aliangalia kidogo tu nyuma. Na kama . . . Mungu alimgeuza mtu huyo mwenye haki, Lutu, mke wake, akawa nguzo ya chumvi, kwa kitu kidogo tu, kutozitii tu Amri Zake vya kutosha kuangalia nyuma na kuona huo moto wote ulikuwa unahusu kitu gani, na yeye akageuka akawa nguzo ya chumvi, nayo bado inasimama pale siku hizi kama mfano ya kwamba Mungu humaanisha anayosema.

⁸³ Loo, laiti imani halisi ingalitia nanga ndani ya watu! “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu.”

⁸⁴ Hawa alisimama kwa muda kidogo. Hivyo ndivyo tu ilivyompasa kufanya. Shetani akamnasa, na kuhojiana tu naye, “Hilo si ni la maana? Kama Dada *Fulani* anaweza kufanya hivyo, hivi wewe huwezi kufanya hivyo, pia? Yeye ni mke wa mchungaji.” Sijali mwanamke huyo ni nani, ama mwanamume huyo ni nani. Kama ni kinyume na Neno, kamwe usisikilize. Nenda moja kwa moja! Mifano!

⁸⁵ Hivyo ndivyo Ibrahimu alivyofanya. Unafikiri ni hoja kiasi gani sa—sayansi ya tiba ingaliweza kumpa, ya siku hiyo, ya kwamba asingempata mtoto huyo? Na vipi wakati alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano? Kisha tunamwona wakati alipokuwa na mia moja, angali aliliamini kwa dhati zaidi

kuliko alivyofanya hapo mwanzoni, alikuwa na miaka ishirini na mitano ya kuendelea kujenga imani zaidi kwa jambo hilo. Ninapenda jambo hilo. Naam, bwana.

⁸⁶ Halafu ninataka kuuvutia usikivu wenu kwenye jambo lingine kabla hatujasimama. Je! mliiona? Na—natumaini kwamba mlilipata. Juu ya hilo agano kuthibitishwa, kwa kuliandika agano hilo na kulirarua vipade viwili, je! mlilipata? Inueni mikono yenu kama mlilipata, mlipata maana yake. Agano liliandikwa, likapasuliwa, Mungu akichukua dhihirisho la utatu, akiufanya kuwa mmoja; akaurarua vipande viwili, akaupoleka ule mwili kule Juu, na kumrudisha Roho Mtakatifu apate kuishi katika Kanisa, kutoa kitu kile kile kilichotolewa na huo mwili, kama mke, Bibi-arusi; Roho yeye yule, kazi ile ile, Fundisho lile lile, kila kitu vile vile hasa alivyofanya, ishara ile ile, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Angalia!

Huenda kukawepo, labda, Myahudi anayeketi hapa.

⁸⁷ Unaona, Mungu hufanya mambo hayo, na linaendelea moja kwa moja miongoni mwa watu na bado hawalipati.

⁸⁸ Kama vile nilivyokuwa nikielezea kwa nini wanawake hufunika uso wao wanapofunga ndoa. Ni kwa nini? Huenda wasifahamu jambo hilo. Lakini kile wanachofanya, ni, wakijua ya kwamba wao ni mwili, hawana kichwa, mwanamume ndiye kichwa chao. Hiyo ndiyo sababu Rebeka alijifunika. Na hiyo ndiyo sababu Kanisa linapaswa kujifunika na kujisalimisha kwa Kristo, kwa sababu Yeye ndiye Kichwa, na Yeye ni Neno.

⁸⁹ Sasa, Wayahudi, ile Yom Kippur, wakati wanapokula ushirika, ama Pasaka, mtu yeyote anajua, ambaye ni Myahudi, na anajua kwamba chini ya kifuniko hicho kuna kipande kidogo cha mkate mwembamba uliovunjwa. Wala hakuna Myahudi ninayemjua, ambaye nimewahi kuzungumza naye, anayeweza kueleza ni kwa nini hicho kipande kilichovunjwa cha mkate mwembamba. Mbona, hii hapa katika kuthibitishwa kwa agano hilo, ule mwili wa Kristo uliovunjwa, wakati alipomtenganisha Mungu kutoka kwa mwanadamu; Yeye alikuwa Mungu na mwanadamu pia. Na wakati alipompeleka Roho juu... Ndipo Yesu akasema, sikilizeni, “Katika siku hiyo mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba, Baba ndani Yangu; Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu.” Ni Mungu katika watu Wake! Mungu yeye yule!

⁹⁰ Yeye aliwakilisha pale, mahali tulipozungumzia jana usiku. Mungu alishuka chini, herufi kubwa B-w-a-n-a, Yehova-Yire, Yehovah-rafa, Yehova-manase, Elohimu, Yeye Ajitoshelezaye kwa Yote, yule Mwenye Nguvu, Mwenye Maziwa, sifa Zake zote na kila kitu, akidhihirishwa katika mwili wa binadamu uliokula chakula cha binadamu, na kutoweka machoni pao. Mungu!

⁹¹ Na Yesu, wakati alipokuja, Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku hiyo, ndivyo itakavyokuwa.” Mungu!

⁹² Huo ni ule mkate mwembamba uliovunjwa chini ya kifuniko, kile kipande kilichovunjwa, si kile wanachokula, bali Kile kilichovunjwa. Ni kwa nini hawalifahamu?

⁹³ Ni vile vile wakati Yesu alipoyachukua yale—yale magombo na kuanza kuyasoma. Yeye alisoma sehemu ya kifungu hicho, kisha akaacha, yaliyosalia, kwa maana yalikuwa ni Yake tu kwa ajili ya siku hiyo. Sehemu iliyosalia ya kifungu hicho ilihusu Kuja Kwake Mara ya Pili.

⁹⁴ Hiyo ndiyo sababu Wayahudi hawaelewi jambo hilo, kwa sababu ilibidi wapofushwe. Hawakumwona Masihi wao, na hata hivyo alikuwapo. Na kila wakati wanapokula Pasaka ya—yao, huo hapo ule mkate mwembamba tena uliovunjwa, wala hawajui jambo hilo.

Nilimwuliza rabi mmoja. Akasema, “Tumefundishwa kufanya hivyo.”

Nikasema, “Mbona mnafanya hivyo?”

Akasema, “Sijui. Hakuna mtu mwingine ajuaye.”

⁹⁵ Unaona, mwanamke huufunika uso wake, hata hivyo yeye hatambui. Badala ya kuingia na kumwacha mumewe awe kichwa chake, yeye ndiye kichwa cha mumewe. Huo ni upotovu. Sasa hivyo ndivyo ilivyo tabia ya Marekani.

⁹⁶ Lakini jambo ndilo hilo, mkate mwembamba uliovunjwa. Ndipo tena tunaona, tena nilitaka mwone hapa, katika kuuwekea msingi sasa kabla hatujaingilia sehemu halisi tunayotaka kuzungumzia usiku wa leo.

⁹⁷ Jana usiku mnakumbuka ya kwamba wakati Ibrahimu, lile agano lilipofanywa pamoja na Ibrahimu na Uzao wake baada yake. Sasa, kulikuwa na uzao wa maumbile ya kawaida wa Ibrahimu, kwa tendo la imani liliuleta huo; bali Uzao halisi wa Ibrahimu ulikuwa ni Kristo, Biblia. . . ambao ulikuwa ndio Uzao wa kifalme wa Ibrahimu. Sasa angalia.

⁹⁸ Ibrahimu, kabla ya yale maangamizi ya moto katika siku yake, kulikuwako na ishara aliyofanyiwa Ibrahimu, kundi Lake teule. Na hiyo ilikuwa ni, Mungu alishuka katika umbo la mwanadamu, akielekeza mgongo wake hemani ambamo Sara alikuwa, na akasema yale Sara aliyokuwa akisema hemani. Na Yesu akaja na kusema jambo lile lile lingetukia katika mwisho wa wakati. Sasa, huyo alikuwa ni Ibrahimu.

⁹⁹ Ndipo uzao wake wa kawaida, Masihi ajapo. Naye Simoni akaja kwa Yesu, na Yeye akamwambia jina lake lilikuwa ni Simoni, naye alikuwa mwana wa Yona, akijua siri ya moyo wake. Alimwambia Filipo. . . ama Nathanaeli, aliyetwa na Filipo, “Nilikuona ulipokuwa chini ya ule mti.” Akamwambia yule mwanamke pale kisimani, “Ulikuwa na waume watano”; naye akasema, “Bwana, naona kwamba Wewe u nabii.” Unaona, mwisho wa uzao wa kimwili wa Ibrahimu ulipata ishara hivyo.

¹⁰⁰ Na ilibashiriwa na Uzao wa kifalme Mwenyewe, Kristo, ya kwamba Uzao wa kifalme, katika mwisho wa siku zao, ungepata jambo lile lile. Sasa ninatumaini tunalipata.

¹⁰¹ Akambadilisha. Angalieni, Mungu alilibadilisha jina la Ibrahimu. Afadhali niachilie jambo hilo hapo. Nitakaporudi kwa ajili ya uamsho mrefu, tutaingilia jambo hilo. Ilimbidi kulibadilisha jina lake kutoka kwenye jina lake la duniani, kuwa jina lililotolewa na Mungu.

¹⁰² Mnasema, “Jina lina uhusiano gani na chochote?” Loo, ndugu, laiti ungalijua! Kwa nini, baadhi ya haya majina ya kisasa tuliyo nayo! Sitaki kuyataja, maana itawaudhi. Bali Mungu ana majina ambayo yanamaanisha mambo, inabadilisha mwelekeo wote. Loo, unasema, “Upuuzi!

¹⁰³ Vipi kuhusu—vipi kuhusu Yakobo? Kabla hajafanyika mtawala mbele za Mungu, ilibidi jina lake libadilishwe kutoka Yakobo liwe Israeli. Hiyo ni kweli? Hakika. Paulo; Sauli ilibidi abadilishwe jina lake liwe Paulo. Loo, ni wangapi tungaliweza kuwataja, na kusema ya kwamba Mungu alibadilisha jina lao! Abramum likawa Ibrahimu, Sarai likawa Sara, akibadilisha jina lao. Loo, jamani! Ni baraka jinsi gani, kuingia katika maskini kanisa dogo pamoja na kundi la wateule, na kuanza kufundisha hayo, kuona haleluya moyoni, unapoona yale Mungu anayofanya.

¹⁰⁴ Sasa, jana usiku nilikuwa nikieleza juu ya “katikati ya mstari” na “kulithibitisha.” Ninataka tu kuligusia tena kabla sijaingia kwenye somo langu. Ya kwamba, Mungu alimbadilisha Ibrahimu kutoka mzee aliyejaa makunyanzi, yeye na Sara, akawarejesha kuwa mume na mke vijana, akaibadilisha miili yao kabla hawajampokea mwana aliyeahidiwa. Ishara ya mwisho waliyoipata ilikuwa ni udhihirisho wa Mungu katika mwili, angeweza kuusoma moyo wa mwanamke aliye nyuma Yake, hemani. Na jambo lililofuata lilikuwa kwamba miili yao ilibadilishwa. Sasa, jana usiku nilikuwa nikichelewa, nami ningeweza kuwasikia wengine wakishangazwa nalo. Ninataka kuendelea kulileta karibu zaidi kidogo.

¹⁰⁵ Sasa, thibitisho la jambo hilo lilikuwa ni kwamba, wakati wote wawili walipofanya safari hiyo ndefu, walikuwa wamebadilishwa kabisa. Na Biblia ilisema, “Wote wawili walikuwa na umri mkubwa. Na mwili wa Ibrahimu ulikuwa kama uliokufa, na tumbo la uzazi la Sara lilikuwa limekufa.” Hiyo ilikuwa ni kweli? Tunajua walikuwa wamekufa, bali Mungu aliwabadilisha. Sasa kuwathibitishia jambo hilo, ya kwamba Yeye aliwabadilisha. Kwanza, kwa nini huyo Mfilisti (ama si ninii...), naam, ninaamini alikuwa ni mfalme wa Kifilisti, akampenda Sara, mwanamke mkongwe? Naye alikuwa ni mrembo wa sura.

106 Jambo lingine. Wakati Isaka alipozaliwa, na Sara na Ibrahimu wana umri mkubwa, wakiwa tayari kufa, ndipo wakaishi, naye Isaka akaoa wakati akiwa na umri wa miaka arobaini; Sara akafa. Na Ibrahimu akamwoa mwanamke fulani, Ketura, kisha akazaa wana watano, sita, ninaamini walikuwa sita, mbali na mabinti, baada ya hapo; na hapa, miaka sitini iliyopita, yeye alikuwa kama mtu aliyekufa! K-e-t-u-r-a-h, Keturah. Alimwoa Keturah, miaka hamsini ama sitini baadaye, naye akawazaa wana sita mbali na mabinti wake; na miaka sitini hapo kabla, alikuwa kama mtu aliyekufa. Haleluya! Haya basi! Ahadi ya Mungu ni ya hakika. Amina. Loo, ninapenda jambo Hilo!

107 Kukaa peke yako tu na kusoma! Leo hii, huko nyuma mwituni, nikisoma, nilipata jambo fulani dogo ninalotaka kuelezea.

108 Israeli. Watu wa Mungu siku moja walikuwa huko chini Misri, wameuzwa katika utumwa, wala wasingeweza kujizuia kuwa kule. Mpango mkuu wa Mungu uliokusudiwa tangu zamani uliwapeleka kule. Yeye alikuwa amemwambia Ibrahimu wangekaa katika nchi ya kigeni kwa muda wa miaka mia nne. Na huko wakawa kama watu wengine, nao walikuwa ni watumwa. Kama—kama mwanamume Mmisri alitaka kuwabaka wasichana wadogo wa Kiebrania, hakuna jambo lingalisemwa. Kama walitaka kuwaua vijana wao wanaume, waliwaua, hakuna kitu kingeweza kusemwa. Walikuwa ni watumwa. Waliwatupia mikate yao iliyoingia kuvu. Wakaila, ama wakae bila; wakilalamika, wanauawa! Ni mahali pa namna gani kwa watu wa Mungu!

109 Lakini siku moja, haleluya, Mungu aliikumbuka ahadi Yake kwa Ibrahimu. Utukufu! Sasa ninaanza kujisikia wa kidini tena. Angalieni, Mungu aliikumbuka ahadi Yake kwa Ibrahimu. Ndipo akamtia mafuta nabii, akiwa na Nguzo ya Moto juu yake, ndipo akashuka akaingia nchini na kuanza kuwakumbusha juu ya ahadi ya Mungu isiyoweza kushindwa. Na Mungu alikuwako kulithibitisha Neno Lake. Naam. Yeye aliwaambia kuhusu nchi iliyokuwa imejaa maziwa na asali, Mungu alikuwa amewapa hiyo. Wakatoka Misri juu ya nguvu za ushuhuda wa nabii huyu mwenye Nguzo ya Moto juu yake, kwa sababu alikuwa ametumwa. Na Mungu alikuwa amethibitisha ya kwamba alikuwa pamoja naye.

110 Sasa walipofika mahali panapoitwa Kadeshi-barnea. Hapo wakati mmoja palikuwa ndipo kiti cha hukumu cha ulimwengu, Kadeshi-barnea. Na hapo walikuwa na shujaa miongoni mwao, jina lake Yoshua. Nalo jina *Yoshua*, katika Kiebrania, linamaanisha “Yehova-mwokozi.” Na Yoshua, yule shujaa mkuu... Sasa kumbukeni, hawakuwa wameiona nchi hii kamwe, walikuwa tu wamesikia habari zake. Mnauona huo mfano wake sasa? Ila tu walikuwa wamesikia habari za

nchi hiyo. Walikuwa wameacha yote wapate kwenda kwenye nchi hii, kwa maana walikuwa wameletewa Neno la Bwana, na kuthibitisha ya kwamba walikuwa njiani wakienda zao kwenye nchi hii. Ni mfano wa jinsi gani wa Kanisa, likiwa njiani likienda zake, bila kujua lolote kuihusu, hakuna mmoja wao aliyewahi kuwa huko. Lakini Yoshua, walipoukaribia ule mpaka, huko Kadeshi, kile kiti cha hukumu, ambapo hukumu iliipiga Israeli, kutoka kwa mtu aliyekuwa ameingia mle na kurudi. Na Yoshua alivuka Yordani, akaingia kwenye nchi ya ahadi, na akaleta ushahidi ya kwamba ilikuwa vile vile hasa Mungu alivyosema ilikuwa. Nao wangeweza kuonja zile zabibu zilizokuwa zimekuzwa kwenye nchi hiyo ya raha.

¹¹¹ Sasa, walikuwa wameahidiwa ya kwamba wangeweza kuwa na nyumba ambapo wangekuwa huru, wangewalea watoto wao katika adabu na—na hofu ya kiungu, wawe na kanisa, na kadhalika. Walikuwa na furaha jinsi gani kuvuka nchi hiyo na kupata makazi haya, kutoka kuwa watumwa. Angalieni. Lakini walipovuka, wakaishi maisha yao, lilikuwa ni jambo kubwa. Lakini hatimaye miimba ya vilima ikajaa mawe ya makaburi. Walizeeka na wakafa, wakazeeka na kufa, watu wa Mungu.

¹¹² Ndipo siku moja akatokea Shujaa mwingine, aliye mkuu kuliko wote, Yehova-mwokozi, *Yesu*, Yeye alikuja, na akasema, “Kuna Uzima baada ya mauti! Kwa maana, Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi. Kama sivyo, ningaliwaambia. Nitaenda na kuwaandalia mahali, na nitarudi tena niwakaribishe Kwangu.” Na Shujaa huyu mkuu akafikia Kadeshi-barnea Yake, kiti cha hukumu kwetu sisi sote, Kalvari! Hapo alijitwalia uovu wetu sisi sote. Kisha akauvuka mto Yordani tunaouita mauti. Na katika siku ya tatu akafufuka tena, kama vile Yoshua alivyovuka ule mto akarudi, akileta ushuhuda ya kwamba “mtu aliyekufa anaweza akaishi tena.”

¹¹³ Naye akasema, kufanya ninii yenu...kuwahakikishia, “Ninawatakeni mpande mwende kule kwenye mji wa Yerusalemu, mkangoje kule. Nitawapa arabuni Yake. Nitawapa ushuhuda, yale malipo ya kwanza.” Nao wakapanda wakaenda mjini Yerusalemu na kungoja mpaka Uzima wa Milele ukaja kama upepo wa nguvu ukienda kasi.

¹¹⁴ Na leo hii, baada ya miaka elfu mbili, tungali tuna ushuhuda huo ya kwamba tumepita toka mautini kuingia Uzimani. Yoshua wetu ametuletea ushuhuda, nasi tuko njiani tukielekea kwenye Nchi hiyo ya ahadi, tukivionja vipawa vya mbinguni vya Mungu ambavyo ametuletea. Angalieni, jinsi ilivyo ya ajabu! Angalia mahali ulipokuwa wakati mmoja. Mlevi... .

¹¹⁵ Nilikutana na ndugu mmoja leo; nilipata hisi ya kigeni kugeuka kuingia kwenye mtaa fulani, na kuondoka. Ninasahau jina la mtu huyo lilikuwa ni jina gani. Huenda akawa yupo hapa mkutanoni. Hata hivyo, kama hayupo, mbona, Mungu alikuwa

ni mwema kwake. Yeye ni Mhindi, nusu Mhindi. Ametokea Virginia. Roho Mtakatifu aliniambia, si kulisema. Nilikuwa nimemwacha mke wangu atoke. Kasema, shuka uende *hivi*, kisha ukate kona *hii*.” Nikashuka kwenda kule chini. Loo, linatukia wakati wote. “Ngojea papa *hapa*.” Ndipo nikangojea hapo dakika chache. Kasema, “Geuka urudi juu *hivi*.” Na, nilipofanya hivyo, nikakutana naye.

¹¹⁶ Akasema, “Ndugu Branham, ninakujua.” Kasema, “Nilikuja Jeffersonville wakati mmoja, na kukutafuta.” Nami nikasema... “Ulikuwa umeenda ng’ambo.” Lakini alikuwa ni mlevi, maishani mwake. Nikaushika mkono wake, bila yeye kujua nilichokuwa nikifanya. Naye alikuwa na sirosisi ya ini. Nilipokuwa nimesimama pale nimeushika mkono wake, mtetemo ukaniacha. Ni kitu gani? Aliponywa. Papo hapo pembeni mwa mtaa, wanasikia jambo hilo mjini mwenu.

¹¹⁷ Sijui mtu huyo alikuwa ni... Je! yupo hapa? Sijui. Kama yupo, yeye... Si—sijui. Yeye alisema a—alikuwa akitaka kurudi nyumbani. Nafikiri ilimbidi kwenda. Alikuwa M—Mhindi, nafikiri alikuwa amemwoa mwa—mwanamke mzungu. Naye alikuwa anatokea Virginia. Nami ninasahau jina lake anaitwa nani. Aliishi hapa chini karibu na Logar ama kitu kama hicho. Naye alikuwa ameenda mpaka Jeffersonville. Lakini alijisikia kutembea pembeni, Roho Mtakatifu akasema, “Shuka uende *huku*.” Ee Mungu, uturehemu! Haya basi.

¹¹⁸ Ningeweza kuchukua saa kadhaa baada ya saa kadhaa, kuwaambia mambo ambayo nimeyaona yakitukia na kufanywa namna hiyo. Kwa nini? Yesu, Shujaa wetu mkuu, alivuka na kuiteka nchi, akaishinda mauti, akakushinda kuzimu, akalishinda kaburi, akafufuka siku ya tatu, na kusema, “Mimi Ndimi ndimiyekwa nimekufa, na ni hai tena milele na milele, na nina funguo za mauti na kuzimu.” Huyo hapo yule mshindi, tangu alipolipasua lile pazia vipande viwili. Huyo hapo amesimama!

¹¹⁹ Ni kama vile maskini dada mmoja mweusi mkongwe. Samahani, rafiki zangu weusi mlio hapa ndani. Yeye alikuwa akitoa ushuhuda mkutanoni, naye alikuwa ni wa kusini sana katika matamshi yake. Akasema, “Vema, ninataka kuwaambia ninyi nyote jambo fulani usiku wa leo.” Akasema, “Hakika siko vile ninavyopaswa kuwa.” Kisha akasema, “Hakika siko vile ninavyotaka kuwa. Bali jambo moja nijualo, siko vile nilivyokuwa.” Kwa hiyo alikuwa amekuja mahali fulani!

¹²⁰ Nami nasema, ndivyo ilivyo usiku wa leo! Wakati mmoja tulikuwa tumepotea katika dhambi. Na leo hii, kwa kuukubali ule ushuhuda, ile ahadi iliyorudishwa (malipo ya kwanza ya wokovu wetu wa Milele), tumefufuka kutoka mautini tukaingia Uzimani, na tunaishi juu yake. Itakuwaje wakati tutakapopata

malipo yote, na kuuvuka ule mto, sisi wenyewe, tuingie kwenye ile Nchi tukufu?

¹²¹ Majaribu makuu! Sasa Ibrahimu, baada ya mambo haya yote ya ajabu, yeye alijaribiwa baada ya kuipokea baraka. Ibrahimu alijaribiwa.

¹²² Sasa hapo ndipo watu wanaposhindiwa. Sasa, sikilizeni kwa makini sasa, msilikose. Biblia ilisema, ya kwamba “Kila mwana amjiaye Mungu hana budi arudiwe, kurudiwa, kupigwa. Na kama hatuwezi kuyastahimili marudio, tunakuwa watoto haramu, wala si watoto wa Mungu.” Inathibitisha ya kwamba imani yetu haikuwa jinsi tulivyosema ilikuwa, hatuna kile tulichojidai kuwa nacho. Sasa tunaingia kwenye namna ya Ukalvini mzuri kweli sasa, kwa hiyo inatupasa kuangalia jambo hilo. Sasa angalia, “Kila mwana amjiaye Mungu hana budi arudiwe, kurudiwa,” Neno humpiga na kumkata vipandevipande, kupiga kila kanuni ya imani iondoke chini yake; unaona, kujaribiwa, na kuona kama yeye ni mwana wa Mungu.

¹²³ Sasa Ibrahimu, baada ya kuipokea ile baraka, basi alijaribiwa baadaye.

¹²⁴ Wakati huo unaenda wapi? Hata sijamaliza somo langu, na ni wakati wa kufunga. Je! mtanivumilia kwa dakika zingine kumi na tano? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Asanteni. Iweni na kicho. (Ibrahimu. Mwangelieni Nuhu.) Hebu tulichukue tu kwa dakika moja. Hatuwezi kuharakisha; hakuna haja. Na, jamani, kwa nini tuharakishe? Mimi huenda polepole. Mimi—mimi si kama baadhi ya jamaa hawa wanaoweza kusimama, wanaweza tu kuliharakisha tu namna hiyo. Mimi—mimi—mimi ni mwenda pole, sina budi kungojea mpaka atakaponipa jambo.

¹²⁵ Mwangelieni Nuhu, baada ya Mungu kumfanya ahubiri miaka mia moja na ishirini, moja kwa moja katikati ya ulimwengu mkuu zaidi wa kisayansi kuliko tulivyo nao leo. Loo, hakika, walijenga mapiramidi. Tusingeweza kuyajenga. Walijenga sfinksi. Tusingeweza kuijenga. Walitia miili dawa kuifanya ionekane haijharibika idumu hivyo hata siku hizi. Hatuwezi kufanya hivyo. Walikuwa na rangi ambayo wangeweza kuiweka katika vitu mbalimbali, hata rangi hiyo haikubadilika kwa miaka elfu nne. Hatuna hiyo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Nayo ilionyesha ya kwamba walikuwa na ustaarabu kama ule Yesu aliosema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu.” Naye Nuhu, katika ulimwengu huo wa kisayansi, akihubiri, “Mvua itanyesha kutoka mbinguni, kwa sababu Neno la Mungu lilisema hivyo!” Nuhu alikuwa ni nabii.

¹²⁶ Na mnapowaona manabii wakitokea, afadhali mwangelie, hukumu iko njiani.

¹²⁷ Kwa hiyo basi Nuhu akihubiri, nao watu wakiukataa, wakamcheka usoni mwake. Naweza kuwazia wengine wao

walisema, “Jambo hilo halikidhi kibali chetu cha kisayansi.” A-ha!

¹²⁸ Ninawazia, ni jambo lile lile kama ilivyo leo. Wao wanasema kwamba, “Kupiga makelele na kumsifu Mungu, na kulia, na haya hapa maisha yanayodhaniwa ni maisha ya ‘watakatifu wanaojifingirisha’ na kadhalika, yote ni mihemko ya kujibunia.” Hayakidhi kibali chao cha kisayansi, bali yanaikidhi Biblia ya Mungu. Hilo ndilo jambo muhimu. Angalieni.

¹²⁹ Ninawazia sayansi ilitoka ikasema, “Angalia, ewe jamaa. Angalia, kwa namna fulani u—umerukwa na akili. Angalia hapa. Mimi, sisi tuna rada, tunaweza kuulenga mwezi ama kuirusha Sputniki huko juu. Hakuna tone moja la maji kati ya hapa na kule. Sasa inatoka wapi?”

¹³⁰ Ninaweza kumsikia Nuhu akisema, “Mungu alisema hivyo! Na kama Mungu alisema ilikuwa hivyo, Yeye ni Yehova-Yire, aweza kuyatoa maji kule juu. Mungu alisema hivyo! Itatendeka, hata hivyo!” Mtu mmoja alisema. . .

¹³¹ Hebu mchukue mtu anayekufa kwa kansa, kivuli cha mtu, huyu hapa; mwaka ujao ni mtu mzima mwenye afya njema. Ilitukiaje? Alimlaza nyuma. . . Nina mamia ya shuhuda hizo. Mtu amekwisha kutoka kwenye maisha haya, daktari akatia sahihi taarifa, “Amekufa, amekufa kwa saa kadha wa kadha.” Ndipo Mungu anatoa ono, na mtu huyo yu hai sasa. Vipi? Usiniulize. Sijui. Bali Mungu alisema, “Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, toeni pepo.” Hiyo ni kweli.

¹³² Wakati wowote unapokuwa mgonjwa na Mungu anatangaza uponyaji, e—endelea tu na daktari wako, acha akwambie wakati utakapokuwa mzima. Atakupa. . . Hilo litatoa ushuhuda kwake. Anaposema, “Vema, wote umekwisha”; sema, “Mungu asifiwe! Asante, daktari, kwa huduma zako,” na uzidi kuendelea. Unaona? Hiyo ni kweli. Angalia.

¹³³ Sasa Nuhu, yeye alisema, “Mvua inakuja, ulimwenguni kote, itawafagilia mbali ninyi watu waovu.”

¹³⁴ “A-ha, upuuzi! Tuna makanisa yetu. Mchungaji wetu hasemi kitu kama hicho. Huyu mzee amerukwa na akili, akijenga safina kule juu. Unafikiri mtu yeyote ataamini jambo hilo?”

¹³⁵ Siku moja, Mungu akasema, “Nimesikia dhihaka zao za kutosha. Niko tayari sasa. Ingieni!” Nao hawa hapa wanyama wanakuja, wawili wawili, kasuku wa kiume na wa kike, shorewanda wa kiume na wa kike, mbuzi wa kike na wa kiume, kondoo wa kiume na wa kike, simba, chui milia, wote wanaopumua pumzi duniani, wakaingia safinani.

Nuhu akasema, “Hiyo ndiyo ishara yenu ya mwisho!”

¹³⁶ Nao wasingeliamini. “Panda juu uende ukaishi na wanyama wako wanaonuka.”

¹³⁷ Huyo hapo, Nuhu akimtii Mungu. Haidhuru ulimwengu ulisema nini, yeye alimsikiliza Mungu; alikuwa ni nabii. Aliingia katika safina, ndipo Mungu akafunga mlango nyuma yake.

¹³⁸ Sasa ninaweza kuwazia, baadhi ya waaminio wakwamia mpakani, walioketi hapo karibu na kuusikiliza ujumbe wa Nuhu, na kuondoka mmoja mmoja, unajua, walisema, “Unajua nini, huenda mzee huyo alisema kweli. Hebu tupande twende huko juu tukasimame karibu. Akasema, ‘Mvua itaanza kunyesha mlango huo utakapofungwa.’ Mungu alimwambia Yeye ataufunga mlango, itanyesha. Hebu na tupande twende huko tukasimame karibu. Na kama ikianza kunyesha, tutabisha mlango. Kwa sababu yeye ni mzee mwenye huruma, atafungua mlango.”

¹³⁹ Unaona, wakati mwingine unamwangalia mjumbe badala ya Ujumbe. Mungu alifunga mlango. Haidhuru Nuhu alikuwa mwenye huruma jinsi gani, Mungu ndiye aliyefunga na kufungua, chochote anachotaka.

¹⁴⁰ “Ndugu Branham, kuna mtu anayeketi hapa chini pembeni. Shuka uende ukamponye, tutaamini katika uponyaji wa Kiungu.” Huyo ni ibilisi.

¹⁴¹ Yuyo huyo aliyesema, wakati walipoweka kitambaa usoni Mwake na kumpiga kichwani, barazani, alisema, “Kama wewe ni nabii, twambie ni nani aliyekupiga sasa. Tutaamini.” Yeye hamfanyii mtu yeyote vitimbi. “Ikiwa Wewe ni mwana wa Mungu, geuza mawe haya yawe mkate. Kama Wewe!” Yeye angeweza kufanya hivyo, bali hamfanyii mtu yeyote vitimbi. “Kama wewe ni mwana wa Mungu, shuka utoke msalabani.” Makasisi walikuwa wakisema hivyo, unaona. Hakumfanyia mtu yeyote vitimbi.

¹⁴² Alifanya tu jinsi Baba alivyomwonyesha, na si kitu kingine tofauti. Hivyo ndivyo alivyosema, Yohana Mtakatifu 5:19, “Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda.” Haya basi. Angalia.

“Tutapanda twende tukasimame karibu na safina, kama ikianza kunyesha. . .”

¹⁴³ Ninawazia Nuhu alisema. . . Aliingia kwenye safu ya kwanza, akapanda hadi kwenye safu ya pili (ndege) kutoka kwenye vitu vitambaavyo, hata kwenye ofisi iliyofuata. Kutoka kwenye kuhesabiwa haki, hadi kwenye kutakaswa (ndege), kisha akatoka hapo akaingia kwenye Ubatizo wa Roho Mtakatifu; mahali dirisha lilipokuwa, ambapo nuru ingeweza kuingia. “Nimepanda juu mbinguni, nikaketi.” Kasema, “Vema, familia, ninyi mliongia humu ndani pamoja nami, asubuhi. . . Nachelewa alasiri ya leo sasa. Sasa Mungu alifunga mlango kule chini. Asubuhi, kutakuwako na giza kote duniani. Asubuhi, mvua itaanza kunyesha na safina itaelea, na Mungu ata—

atamwangamiza kila mmoja wa hao wenye dhambi wakatili ambao wameukataa Ujumbe.” Wote wakingojea.

¹⁴⁴ Kesho yake asubuhi, wakaamka, wakaangalia nje, kuzuri na kumetakata. Akaingia safinani, ni wangapi wanaojua aliingia ndani siku gani? Siku ya 17 ya Mei, wakati Nuhu alipokuwa na umri wa miaka mia sita. Siku ya 17 ya Mei, Biblia ilisema hivyo. Na wakati alipoingia, siku ya 17 ikapita, jua likachomoza kali tu kadiri lilivyowahi kuwa.

¹⁴⁵ Ningewawazia hao, wakwamia mpakani, wakisema, “A-ah! Niliwaambia hamna kitu hapo! Kwa nini ninyi nyote mnazubaa hapo? Ondokeni hapo kwa bingwatapeli kama huyo!”

“Vema, nafikiri hiyo ilikuwa ni kweli.”

¹⁴⁶ Lakini, unaona, kuna mstari wa kugawanya uliochorwa kati ya kuamini na kutokuamini. Nawe ama unakuja upande mmoja ama huo mwingine. Na upo wakati utakapopokea wito wako wa mwisho.

¹⁴⁷ Kwa hiyo, siku ya pili, ilikuwa ni kuaibika jinsi gani kwa Nuhu na kanisa lake, wakati alipowaambia Mungu atauangamiza ulimwengu. Lakini mnajua alingojea kwa muda gani? Siku saba, hakuna kitu kilichotukia. Kujaribiwa!

¹⁴⁸ Basi katika siku ya nane, kulikuwa na giza ulimwenguni kote, matone makubwa mno yakaanza kuanguka kutoka mbinguni, maji yakaanza kumwagika, na vijito vilianza kufurika. Mitaa ilijaa maji. Watu wakabisha mlangoni, bali Nuhu asingeweza hata kuwasikia. Nayo ikaelea juu ya kilima kilichokuwa kirefu kuliko vyote, na wote waliokuwa nje ya safina wakaangamia.

¹⁴⁹ Mungu akimjaribu Nuhu, kuona kama angejaribu kupanda atokee dirishani, ama chochote kile. Baada ya Yeye kutoa ahadi, Nuhu alivumilia!

¹⁵⁰ Jambo ndilo hilo! Wakati umeipata ahadi, na unajua ya kwamba ni ahadi, dumu nayo! Ilibidi Ibrahimu ajaribiwe. Dumu na ahadi!

¹⁵¹ Sasa, walipata ishara yao ya mwisho. Ndipo mwili wao ukabadilishwa. Na mara mtoto Isaka akatokea jukwaani, mvulana mdogo wa kupendeza wa Kiyahudi. Ningewazia baada ya siku zake nane alitahiriwa. Jinsi mama huyo mdogo, mwenye umri wa miaka mia moja. . . Jinsi ambavyo Ibrahimu, umri wa miaka mia moja; mkewe hasa ana tisini, naye mia moja; jinsi ambavyo hapana shaka walikuwa kwenye, kwenye umri wao wa miaka ishirini na, wakishangilia. Maskini jamaa huyu mdogo, jinsi alivyokuwa wa kupendeza!

¹⁵² Nanyi mwajua, Mungu alisema, “Sasa kuwafanya watu katika siku zijazo (Uzao wa Ibrahimu) ujue, Uzao wako ujue ya kwamba Mimi hudumisha ahadi Yangu kwa mtu yeyote atakayelishikilia Neno Langu, nitampa jaribio.”

¹⁵³ Wakati huyo mvulana mdogo alipofikia umri wa karibu miaka kumi na minne. Nawazia, maskini nywele za matimutimu na macho madogo ya kupendeza. Loo, jinsi ambavyo huyo baba mwenye furaha na mama! Mnajua jinsi ninyi wazazi mnavyojisikia na mtoto wenu, mtoto wa pekee. Ndipo Mungu akamwambia Ibrahimu...Sasa, Yeye asingemwambia Sara, kwa maana Sara alikuwa ndiye chombo dhaifu. Na kwa hiyo akasema, “Ibrahimu, ninataka umchukue mvulana huyu mdogo niliyekupa, yule ambaye nitakufanya baba wa mataifa mengi kwake, nami ninataka umpandishe kwenye mlima nitakaokuonyesha usiku wa leo katika ono, na hapo umwue.” Kuangamiza tumaini pekee lililokuwapo kwake kuwa baba wa mataifa, kwa ajili ya Mungu kutimiza Neno Lake; Mungu alisema, “Nitakufanya baba wa mataifa.” Amengojea sasa miaka hii yote, mpaka yeye ana umri wa miaka mia moja, umri wa miaka mia moja na kumi na nne. “Basi huyu hapa yule mvulana mdogo sasa, na ushuhuda pekee ulio nao ya kwamba nitalitimiza Neno Langu, panda uende ukamwangamize. Ningali nitakufanya baba wa mataifa kwa mtoto huyu.”

¹⁵⁴ “Naye Ibrahimu,” kasema, “hakusita kwenye ahadi ya Mungu. Alijua ya kwamba alimpokea kama mtu kutoka kwa wafu. Alijua, kama Mungu aliahidi hivyo, Yeye angeweza kumfufua katika wafu.”

¹⁵⁵ Halafu ati sisi ni Uzao wa Ibrahimu? Na kosa moja dogo la kitheolojia linaweza kulipuka njiani, kupendwa na wanaume na wanawake hao wengine, unaliendea badala ya kudumu na Neno. Oneni aibu! Dhehebu fulani kubwa, hilo linamaanisha nini kwa Mungu? Yeye atalifagilia mbali namna *hiyo*! [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] Yuko mbali nalo, amekuwa mbali tangu walipounda dhehebu, kila moja ya hilo, na daima atakuwa mbali. Sio watu mmoja mmoja mle ndani, bali mfumo huo wa kimadhehebu, ni kinyume na Mungu. Kila kanisa lililounda dhehebu ni mama...ama ni binti wa dhehebu la Katoliki. Biblia ilisema hivyo, Ufunuo 17, “Maskini yule kahaba wa kale, na binti zake makahaba.” Kweli kabisa.

¹⁵⁶ Tunaye ameketi papa hapa sasa juu ya taifa letu. Oneni aibu enyi Wademokrasia wazuri mliouza haki zenu za mzaliwa wa kwanza! Vema, tutaachilia hilo liende, mpaka nitakaporudi. Angalieni. Ninachelewa. Hivi Kristo wenu hamaanishi zaidi kwenu kuliko siasa zenu? Inawapasa kufanya yale Abraham Lincoln aliyosema. Vema. Angalieni, tunaendelea.

¹⁵⁷ Sasa Mungu alisema, “Mchukue maskini jamaa huyo mdogo, mchukue ukampandishe kule juu ya mlima.”

¹⁵⁸ Sasa mnataka kujua kama Ibrahimu alikuwa ni kijana mwanamume ama hakuwa? Alifanya safari ya siku tatu pamoja na mtoto huyo, na kuni, na mtumishi, na punda. Sasa mtu yeyote, mtu wa kawaida...Nilikuwa nikilinda nyaya za umeme,

nilikuwa nikitembea wakati nilipokuwa bwana nyama, nami naweza kutembea, kwa urahisi, maili thelathini kwa siku. Nasi tuna miguu ya petroli, kama tusemavyo. Lakini watu hao, njia yao pekee ya kusafiria ni kwa miguu, ama kumpanda punda. Nao hawa hapa walikuwa na punda mdogo mwenda pole; nasi tunaweza kumzidi kutembea. Naye huyu hapa, safari ya siku tatu, kisha akakiinua kichwa chake na kuuona ule mlima ukiwa mbali sana, bado. Bila shaka alikuwa umbali wa maili mia moja kutoka kwenye ustaarabu, huko nyuma mbali kabisa nyikani. Sasa sikilizeni, na mwangalie.

159 Ndipo akachukua kuni na kuziweka juu ya mgongo wa Isaka; ule msalaba, Mwana wa Mungu miaka mingi baadaye. Ndipo Isaka akazibeba zile kuni kupandisha kilimani, ambazo alikuwa anaenda kuzilalia kwa ajili ya sadaka. Kuonyesha kivuli kabla!

160 Kama Mungu alitangulia kuonyesha kivuli cha hilo kikamilifu; mke wa Lutu, usigeuke na kuangalia mambo ya ulimwengu. Mifano hiyo yote na vivuli ni vikamilifu. Unaona? Mkumbukeni Hawa. Mkumbukeni mke wa Lutu. Mkumbukeni Lutu mwenyewe, ewe mwanaume. Mkumbukeni, Adamu alijisalimisha kwa mke wake; Lutu, vivyo hivyo. Iweni waangalifu. Ninawaambia tu, kama ndugu. Wakati umeenda kuliko tunavyowazia.

161 Mwangalie maskini mtoto Isaka akipanda kilima. Naye akaingwiwa na mashaka. Naye akaangalia kote kote, na kusema, “Babangu?”

Naye akasema, “Mimi hapa, mwanangu.”

162 Akasema, “Hizi hapa kuni. Na hivi hapa vyote, kila kitu, moto. Bali yuko wapi mwana-kondoo wa sadaka ya kuteketezwa?”

163 Msikilizeni huyo baba mzee, bila tetemeko katika sauti yake, akasema, “Mwanangu, Mungu atajipatia sadaka hiyo.” Mwanawe wa pekee akienda machinjioni, bali hata hivyo huo moyo mzee mwaminifu ulikuwa umejua ya kwamba Mungu hawezi kusema uongo.

164 Huo ndio Uzao wa Ibrahimu leo! “Inawezekaje, Ndugu Branham?” Mungu atajipatia Mwenyewe! “Atajipatiaje?” Sijui. Lakini Yeye ni Yehova-Yire!

165 Akapanda juu kwenye kilele cha kilima, akafingirisha jiwe. Akaweka kuni juu ya hayo mawe, akawasha moto. Kasema, “Isaka, mwanangu, geuka.” Akatoa kamba kutoka kiunoni mwake, akamfunga mikono na miguu yake. Isaka, mtiifu, kama vile Kristo alivyokuwa, hata kufa. Akamweka juu ya madhabahu ya kafara. Akaunyosha mkono wake kwenye ala na kuchomoa kisu chake kikubwa; akakinoa mara chache, akiangalia mbinguni.

¹⁶⁶ “Hakusita kwenye ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu, akijua kwamba alikuwa amempokea kama mtu kutoka kwa wafu, akijua hakika ya kwamba kama Mungu alisema hivyo, kwa kufanya hivyo, angeweza kumfufua kutoka kwa wafu.” Huyu ni Ibrahimu, na huo ni Uzao wake baada yake. Kama huo ulikuwa ni uzao wa maumbile ya kawaida, Uzao wa kifalme unapaswa kuwa vipi? Bila kusitasita! Kile asemacho Mungu, Mungu atakitimiza. Akijua hilo, yeye alishawishika kabisa; ya kwamba yale Mungu aliyoahidi, Mungu aliweza kuyafanya.

¹⁶⁷ Akanoa kisu; macho madogo ya mtoto Isaka yakiangalia hicho kisu kikubwa kikali wakati kikipitishwa juu ya jiwe. Akanyosha mkono nyuma; akarudisha nyuma nywele zake za kipilipili kutoka usoni mwake, akavuta nyuma kidevu chake kidogo. Akauinua, na machozi yakitiririka usoni mwake namna hiyo. Akijua, naye hakusita katika ahadi ya Mungu! Akauinua mkono wake kuchoma kisu hicho katika koo la mwanawe.

¹⁶⁸ Na alipofanya hivyo, sauti ya Mungu ikaita, na kuushika mkono wake, kasema, “Ibrahimu! Ibrahimu, usiunyeshe mkono wako! Ninajua sasa ya kwamba unanipenda Mimi.” Yeye alikuwa akifanya nini? Akiutolea ushuhuda Uzao wa Ibrahimu, baada yake. “Usiunyeshe mkono wako, usimdhuru mtoto huyu! Ninajua ya kwamba unanipenda.”

¹⁶⁹ Na mnamo wakati huo, Ibrahimu akasikia kitu fulani nyuma yake. Naye akaangalia, na kulikuwako na kondoo dume (huyo ni kondoo wa kiume) aliyenaswa kwa pembe zake katika magugu na vichaka. Ndipo Ibrahimu akaenda akamshika huyo kondoo-dume na kumchinja, badala ya mwanawe.

¹⁷⁰ Huyu kondoo dume alitoka wapi? Yeye yuko maili mia moja kutoka kwenye ustaarabu. Mbona, wanyama mwitu wangelimwua kama angalikuwa huko nyuma. Hakika, ni—ni mnyama wa nyumbani. Alitoka wapi? Na, licha ya hayo, alikuwa huko juu sana mlimani, ambako hakuna nyasi wala maji. Na Ibrahimu aliokota mawe kila mahali, ambapo alikuwa, kuitengeza madhabahu. Huyu alitoka wapi? Haikuwa ni ono; alitoa damu. Ono halitoi damu. Haleluya! Yehova-Yire alikuwa amejipatia sadaka Mwenyewe!

¹⁷¹ Wakati Mungu anapochukuliwa katika Neno Lake, Yeye anaweza kutoa chochote anachohitaji. Mungu, Yehova-Yire, angali ni Yehova-Yire usiku wa leo. Yeye ana Dhahihu ambayo imekwishatolewa tayari. Amejipatia Kanisa. Amejipatia Mjumbe, Roho Mtakatifu. Yeye yupo hapa sasa, Yehova-Yire. Bwana amejipatia Mwenyewe Biblia, Roho, Kanisa, Ujumbe, Mjumbe. Na wakati umewadia sasa kwa Kanisa kunyakuliwa na kupeleka nyumbani. Yehova-Yire atatoa njia ya kulitoa Kanisa hilo humu ulimwenguni, kwa kuibadilisha miili hii yetu dhaifu, na kuipeleka juu Utukufuni. Yehova-Yire! Litatimiae

katika siku ya kisasa kama tunayoishi, kwamba mambo haya yatatukia?

¹⁷² Mimi, pamoja na Billy, mwanangu, popote alipo, tulikuwa huko India majuzi tu. Nami nikachukua gazeti. . . Nilipotoka kwenye meli, maelfu walikuwa wamesimama pale wakiwa na mashada ya maua kwa mafungu. Tulipofika kwenye Taj Motel, walikuwa na gazeti pale, katika Kiingereza. Nami nikaona makala makubwa ndani yake, yaliyosema, “Hapana budi ni ishara ya kwamba tetemeko la nchi limekwisha.” Shida ilikuwa ni nini? Vema, yapata siku tatu ama nne kabla ya hilo tetemeko kuu kama mlivyosoma habari zake, maskini ndege wote walioishi kwenye mawe. . .

¹⁷³ Huko India, hawana nyua kama tulizo nazo huku California, Marekani. Wanajenga nyua zao kwa mawe wanayookota. Na maskini ndege wadogo wanajenga viota vyao mle ndani. Wanajenga minara mikubwa, na ndege wanajenga viota vyao mle ndani. Na maskini hao ndege wote, siku chache kabla ya hilo tetemeko kuja, waliruka wakaenda mbali na hizo kuta. Na wakati wa jioni ama. . . Wakati wa adhuhuri, wakati joto lilipoingia, kondoo na ng’ombe wangesimama chini ya kivuli cha ukuta na mnara, kujikinga na jua kali.

¹⁷⁴ Lakini kwa siku mbili, hao ng’ombe na kondoo kamwe hawakuja ukutani. Walisimama huko nje katikati ya uwanja na kuegemeana, wapate faraja. Ndipo tetemeko la ardhi likatokea, likazitikisa na kuziangusha kuta hizo. Basi baadaye maskini ndege hao wadogo wakaanza kurudi, wale ng’ombe kutoka uwanjani. Ilikuwa ni kitu gani? Mungu yeye yule ambaye aliweza kuwaita wale kondoo na ng’ombe, na wale ndege, waingie safinani, alionyesha ya kwamba ni Mungu yeye yule leo anayeweza kuwaita wanyama wake waondoke.

¹⁷⁵ Na kama anaweza kumwongoza mnyama kwa silika, ni zaidi sana jinsi gani Kanisa la Mungu linapaswa kuondoka kwenye kuta hizi kubwa na kujibunia na mafundisho ya makanisa. Babeli itaanguka, moja ya siku hizi. Yehova-Yire amejitandalia Mahali pa Kupumzikia kwa ajili yako. Ruka uondoke kwenye minara ya ulimwengu!

¹⁷⁶ Ruka uondoke kwenye urembo wa Hollywood! Makanisa yanajaribu kuyaiga, kung’aa. Injili haing’ai. Hollywood hung’aa, Injili humeka. Hollywood hung’aa kwa urembo. Kanisa kubwa hung’aa kwa elimu. Nalo kanisa la Mungu aliye hai humeka kwa unyenyekevu na upendo, na Roho Mtakatifu. Ipo tofauti kubwa sana kati ya kumeka na kung’aa.

¹⁷⁷ Yeye yupo hapa sasa. Yehova-Yire amejipatia Mwenyewe. “Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.” Kama madhehebu hayatalikubali, Mungu anaweza kuwaleta watoto Wake kutoka mitaani, makahaba kutoka kwenye mikahawa. Anaweza kuinua chochote anachotaka

kuinua. Lakini kama Mungu ametoa Ujumbe, kuna mtu mahali fulani atakayeupokea. Yehova-Yire! Bwana atajipatia Mwenyewe Ujumbe. Bwana atajipatia Mwenyewe Mjumbe. Bwana atajipatia Mwenyewe, kwa njia Yake Mwenyewe, ishara kwa Kanisa; sio kujiunga, kuweka majina yenu kwenye vitabu.

¹⁷⁸ Tunasikia sana leo kuhusu maamuzi, maamuzi mengi sana. Inafaa nini kulundika mawe kama huna fundi mwashi wa mawe pale kuyakata na kuyaunda yakawa wana na binti za Mungu? Inafaa nini kujenga madhehebu makubwa kwa maelfu, kama humo hamna mtu fulani mwenye upanga wa Mungu ukatao kuwili kuyaunda yakawa watoto halisi wa Mungu? Ni afadhali kuyaacha mahali yalipo. Amina. Mungu (sio Methodisti, sio kama Baptisti, Katoliki), Mungu amejipatia Mwenyewe Kisu cha kuwaunda watoto wa Mungu, wana wa Mungu. Amina. *Yehova-Yire*, “Bwana atajipatia Mwenyewe.” Naye amejipatia! Mwamini, upate kuishi.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo.

¹⁷⁹ Mungu mwenye rehema, Mungu aishiye milele, turehemu sasa, na utupe neema Yako. Hatustahili, Baba, kwa chochote ungetufanyia. Lakini hatukiri ya kwamba tunastahili, bali tunaitikia tu wito kutoka kwa Mungu. Tunaomba, Baba, ya kwamba utatuunda usiku wa leo tuwe mawe yatakayoenea katika Hekalu la Mungu, kwa ajili ya kule Kuja kukuu kwa Bwana Yesu kwenye Hekalu Lake. Tujalie, Baba. Tusamehe sisi wenye dhambi kwa ajili ya kushindwa kwetu. Tufunulie Neno Lako. Tuonyeshe Njia ya kutembea. Tufundishe, Ee Baba, Mungu. Jalia tulipokee. Na kama ni kinyume na Neno, tunajua ya kwamba ni mwalimu wa uwongo. Roho Mtakatifu ndiye mwalimu wetu. Aliliandika Neno, wala asingefundisha chochote ila Neno. Nasi tunaomba ya kwamba atalidhihirisha kwetu usiku wa leo, moyoni mwetu. Tujalie, Mungu.

¹⁸⁰ Sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa, macho yetu yamefumbwa. Neema ya Mungu na iwe juu yetu, ndilo ombi langu nyenyekevu na nyofu. Aminini tu sasa. Msitie shaka.

¹⁸¹ Kuna yeyote humu jengoni, ambamo najua yupo, wanaume na wanawake wasiomjua Yeye, kamwe hawajaikubali Sadaka Yake iliyotolewa, Bwana Yesu, kama Mwokozi wako? Humjui? Huenda kiakili ukadhani unamjua. Bali mtu hawezi kumwona Mungu mpaka amezaliwa mara ya pili. *Kuona* hakumaanishi . . . Huoni kwa macho yako; unaangalia kwa macho yako. *Kuona* ni “kufahamu.” Uliliangalia moja kwa moja, na kusema, “Silioni,” unamaanisha “hulielewi.” Kamwe hutajua kile tunachozungumzia mpaka umezaliwa mara ya pili. Hujapata kuwa na tukio hilo? Huku vichwa vyenu vimeinamishwa sasa, na macho yenu yamefumbwa, ungeweza kuinua mkono wako, na kusema, “Ndugu Branham, nikumbuke katika maombi usiku wa leo. Ninaamini ya kwamba tunaupokea Ujumbe wetu wa

mwisho. Siku inapita haraka. Nami ninaona ya kwamba yale umesema katika Biblia ni kweli, maana nimeisoma Biblia. Ninaamini ya kwamba ndiyo saa ambayo hatuna budi kuja sasa. Na, kwangu mimi, ninachukua msimamo wangu sasa kwa ajili ya Kristo”?

¹⁸² Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe. Vema. Huko juu kwenye roshani, mikono! Inua tu mkono wako, useme, “Kwangu mimi, kama alivyosema Yoshua, ‘Kwangu mimi na kwa nyumba yangu, tutamtumikia Bwana.’” Vema, mtu mwingine? Ninangojea tu. Mungu akubariki huko nyuma. Ninauona mkono wako. Mungu akubariki huko juu. Mungu akubariki. Anakuona. Huko juu kabisa kwenye roshani, Mungu akubariki huko juu, bwana; jambo kubwa kuliko yote ulilopata kufanya maishani mwako. Moja kwa moja kwenye roshani ya katikati, mtu fulani inua mkono wako mle ndani. Labda sikuona mkono pale, huenda ikawa . . . Mtu fulani kwenye roshani hiyo ya katikati huko juu? Inua mkono wako, useme, “Ndugu Branham, kwangu mimi, mimi ni ninii . . . Ninataka kumtumikia. Mimi—mimi ni mwaminifu.” Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki ewe jamaa mdogo. Kwenye roshani mkono wa kulia, mtu fulani inua mkono wako juu huko, na useme, “Ndugu Branham, mimi, kwangu mimi, ninajua hiyo ni kweli. Mimi ni ninii . . . Simjui Mungu, bali ninataka kumjua. Ninataka kuwa na hakika. Ninaona siwezi kubahatisha. Kamwe siwezi kurudi tena.”

¹⁸³ “Jinsi mti unavyoegemea, hivyo ndivyo unavyoanguka,” Maandiko yanasema. Usianguke upande ambao ni njia mbaya. Unaweza kuliweka sawa usiku wa leo. Kumbuka, mradi tu kuna Umilele, na kamwe haukuanza wala hautaisha, bali unakuwa sehemu yake, utateseka ama utaishi kwa furaha. Unajua je utaishi mpaka utakapofika nyumbani?

Unasema, “Mimi ni kijana mdogo sana.”

¹⁸⁴ Ndio kwanza nipate ujumbe juzijuzi. Msichana mdogo huko kwenye mkoa wangu, aligeukia tu njia mbaya, akaanza kuvuta sigara. Alikuwa ameambiwa habari za Mungu, bali asingesikiliza. Umri wa miaka kumi na sita, alikuwa akitoka kwenye ninii yake . . . la, umri wa miaka kumi na minane, ndio kwanza atoke kwenye elimu ya sekondari ya juu. Naye aliambiwa, akijaribu kufanya mema. Bali alianza kuambatana na kundi baya, radi ilimwua mara moja.

¹⁸⁵ Hivi majuzi tu, mtu mweusi huko Shreveport alisimama na kusema, “Hakuna kitu kama Mungu.” Akakufuru tu, kasema, “Hao si kitu ila kundi la watakatifu wanaojifingirisha.” Radi ilimwua. Wakampeleka kaburini. Na walipokuwa wakimzika mtu huyo, kulitokea wingu dogo, na radi ikalipiga jeneza na kumtupa nje ya jeneza hilo.

186 Yehova Mungu hukasirika. Ninajua Yeye ni Mungu mwema, bali ni Mungu wa hukumu, pia. Angali anaangalia, Yeye anajua.

187 Kama wewe huna Mungu, inua mkono wako, useme, “Nikumbuke, Ndugu Branham, unapoomba.” Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, mwanangu. Hiyo ni kweli, njoo moja kwa moja mbele. Mungu akubariki. Hiyo ni kweli, ewe kijana mwanamume. Mungu akubariki huko nyuma. Mwombe Mwenyezi Mungu.

188 Baba yetu wa Mbinguni, sasa umewaona. Unajua kuna mikono ishirini ama thelathini iliyoinuliwa, ya kwamba wanakutaka Wewe kuwa Mwokozi wao. Mungu, tujalie jambo hili sasa hivi. Ninawapa Neno hili. Wewe ulisema, Wewe Mwenyewe, “Yeye alisikiaye Neno Langu.” Nimefanya vizuri nilivyoweza kufanya Nalo, Bwana. “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Ni jambo zuri jinsi gani, kuwazia jambo hilo! Kama mioyo miaminifu nyuma ya mikono hiyo, kweli ilimaanisha jambo hilo, jambo fulani ndio kwanza litukie. Sasa Wewe ulisema, “Kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, Nami nitamkiri mbele ya Baba Yangu na Malaika watakatifu.” Jalia wajue ya kwamba Wewe upo hapa, Bwana. Ninaomba ya kwamba utalijalia. Tusikie. Sisi ni watumishi Wako, Bwana. Katika Jina la Yesu.

189 Vema, inua kichwa chako. Je! mnaamini Yeye ni Yehova-Yire? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Je! mnaamini ya kwamba tuko katika zile siku kama ilivyokuwa katika siku za Lutu? [“Amina.”] Siku za Nuhu? [“Amina.”] Mnakumbuka ule Ujumbe wa mwisho?

190 Yupo mtu hapa kwa mara yao ya kwanza? Inua mkono wako. Wengi! Ninadhani Ndugu Borders amewaelezea. Mmesikia habari za mkutano hapo kabla, kile kinachotukia. Inueni mikono yenu, kama mmesikia; kama hujapata kuliona, ulisikia tu. Vema. Sasa mimi sifahamiani na watu hapa.

191 Baadhi yenu watu wenye shida, mwombeni Mungu, na kusema, “Mungu, unirehemu, mimi ni mgonjwa. Ndugu Branham hanijui mimi. Lakini ninasikia ya kwamba Wewe u Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu.” Ni wangepi wanaojua hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] “Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Mnajua jambo hilo? [“Amina.”] Vema, sasa, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, angefanya nini kama ulimgusa? Vile vile alivyofanya wakati yule mwanamke aliyetokwa na damu alipomgusa. Yeye aligeuka na kumwambia kwamba kutokwa kwake na damu kulikuwa ni nini, na akamwambia imani yake ilikuwa imemwokoa. Hiyo ni kweli? Ni Yeye yule usiku wa leo,

kama unaweza kumwamini vile vile Yeye alivyokuwa wakati huo. Je! unamwamini jinsi hiyo?

¹⁹² Sasa angalieni huku, kwangu. Kama vile Petro na Yohana walivyosema kwenye ule Mlango Mzuri, “Tutazame sisi.” Hiyo haikuwa ni “kuwatazama hao” kwa ajili ya chochote, bali, “kutazama yale waliyokuwa wakisema.”

¹⁹³ Hebu na tuanzie *hapa* mahali fulani. Angalieni huku, na mwamini kwa moyo wenu wote. Na kusema, “Bwana Yesu, ninakuamini, nami ninataka kuligusa vazi Lako. Wewe nena na Ndugu Branham, na umfanye ajue shida yangu ni nini. Nitakuamini Wewe kama utafanya jambo hilo.” Ungefanya hilo?

¹⁹⁴ Sasa hili hapa jambo la ujasiri sana. Ningethubutuje kufanya jambo kama hilo? Ngingekuwa na kasoro fulani kutoa changamoto kama hiyo. Nimetoa changamoto hiyo hapo kabla mbele ya watu nusu milioni, wakati mmoja, nisingeweza hata kuzungumza lugha yao. Bali Yeye hakuniaibisha. Kwa nini? Yeye aliahidi hilo! Hizi ni siku za mwisho, na Yeye aliahidi jambo hili, na ni hili hapa.

¹⁹⁵ Ninajua, enyi marafiki, mmekuwa na mengi sana ya kuwaudhi. Mmekuwa na miigo mingi sana ya kimwili. Bali hebu niwaambieni tu jambo moja, sio kwa faida yangu, bali kwa faida yenu wenyewe. Daima wana jambo hilo. Bali Mungu kamwe hawi na wawili duniani wakati ule ule, hajapata kuwa nao. Lakini kumbukeni tu, kuna miigo mingi sana, bali kuna Mungu halisi. Kuna Roho Mtakatifu halisi. Kuna Ujumbe halisi wa Mungu, na huo ni kwamba Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya wenye dhambi, akafufuka katika wafu, na amerudi katika Utu wa Roho Mtakatifu, kufanya kazi zile zile Kanisani ambazo alizifanya wakati Yeye alipokuwa hapa.

¹⁹⁶ Sasa, hivi Neno la Mungu halisemi jambo hili? Katika Waebrania, lilisema, mlango wa 4, Biblia ilisema ya kwamba, “Neno la Mungu ni kali, lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, likigawanya,” hiyo ni kukata huku na huko, “na hata kwenye mafuta ya mfupa, na Huyatambua mawazo na makusudi ya moyo.” Hiyo ni kweli?

¹⁹⁷ Hiyo ndiyo sababu Yesu aliweza kusimama mbele ya wasikilizaji na kuwaambia. Hao Mafarisayo walisema, “Yeye ni Beelizebuli.” Yesu aligeuka. Hawakusema hilo kwa sauti kubwa ya kusikika, bali Yeye aliwaambia. Hiyo ndiyo sababu Yeye anaweza kumwambia yule mwanamke kuhusu kule kutokwa kwake na damu. Kumwambia yule mwanamke alikuwa ana wale waume; na alipofanya hivyo, ndipo Yeye akasema, “Mbona, hiyo ndiyo ishara ya Masihi.”

¹⁹⁸ Unaona sasa kule kurudi, kule kuonekana kwa Masihi miongoni mwa watu. Ni Roho Mtakatifu akilifanya Kanisa tayari.

¹⁹⁹ Ninataka ugeuze kichwa chako. Unamwona maskini mwanamke yule anayeunyosha mkono pale, akiinuka huku nyuma, anayeketi papa hapa chini? Mnaona ile Nuru iliyo juu yake? Anaugua presha ya juu ya damu. Hiyo ni kweli. Amevaa rinda la bluu, kwa namna fulani amevaa miwani usoni mwake. Kwa sekunde moja iliyoupita, ama mbili, amekuwa akihisi hisi ya kigeni sana yenye joto ikimzunguka. Hiyo ni kweli. Sasa presha yako ya juu ya damu, ambayo imekuwa ikikusumbua sana, imekuacha. Unaukubali? Inua mkono wako kama unaukubali.

²⁰⁰ Yeye aligusa nini? Yule Kuhani Mkuu. Sasa nenda, mwulize mama huyo. Kamwe sijawahi kumwona maishani mwangu. Sijui hata jambo moja kumhusu mwanamke huyo; lakini, hiyo ni kweli. Nilikuwa nikiiangalia hiyo Nuru wakati ikisogea kupitia kusanyiko hili, ilienda kule moja kwa moja kisha ikarudi, Nuru inayomeka.

²⁰¹ Je! unaamini? Yabisi kavu, ugonjwa wa kibofu, magonjwa mengi, wasiwasi, udhaifu. Hiyo ni kweli. Hutokei hapa. Mahali padogo panapoitwa West Point. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia kwamba wewe ni nani? Bi. Hardwick. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako. Yamekuacha. Yesu Kristo anakuponya.

²⁰² Je! mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Naam."—Mh.] Watu wanaangalia upande wa nyuma, kwa ajili yake. Huyu hapa mama huyu ameketi papa hapa. Angalieni, ile Nuru ingali inashikilia juu yake. Hamwioni Hiyo? Hii hapa. Angalieni.

²⁰³ Hiyo hapo, pamoja na yule mtu aliyeketi pale pale akiniangalia. Yabisi kavu. Amini kwa moyo wako wote, Mungu atakuponya, bwana, pia. Sisi hatufahamiani, bali sio kwa Mungu.

²⁰⁴ Mama huyu papa hapa nyuma, anaumwa na kichwa. Mungu, usimwache aukose. Ee Mungu, naomba. Binti Morton, mwamini Bwana Yesu Kristo. Yeye alikuponya kutokana na huko kuumwa na kichwa. Unaona, Yeye asingemwacha apite. Ninataka kukuuliza jambo fulani. Jana usiku wakati nilipozungumza na mtu fulani humu jengoni kuhusu kuumwa kwao na kichwa, ulishikwa na hisi ya kiajabu sana, nawe ulikuwa ukishangaa kama huyo alikuwa ni wewe, ama si wewe. Hiyo si ni kweli? Inua mkono wako. Siyasomi mawazo yako, bali ninakwambia yale umekuwa ukiwazia. Hiyo ni kweli. Leo Yeye alitaka uwe na hakika ilikuwa ni wewe. Kutakuacha sasa, imani yako imekuokoa. Haleluya.

²⁰⁵ Mwangalieni huyu mama anayeketi hapa, amevaa nguo yenye milia. Je! una kadi ya maombi, mama? Angalia yako. Unaamini hiyo henia itakuacha, utakuwa mzima? Unaamini? Inua mkono wako kama hiyo ndiyo shida yako. Vema. Amini kwa moyo wako wote na uponywe. Mnaona ni kitu gani kwangu?

²⁰⁶ Huyo mama papo hapo nyuma yake, aliinua mkono wake, pamoja na ninii dogo. . . la, wa pili hapo nyuma, aliye na maskini nguo inayoonekana ya kijani kibichi, anaugua ugonjwa wa moyo. Naam. Unaamini Mungu atakuponya? Hilo ni sawa, ni zuri. Atakuponya kama utaamini hilo tu.

²⁰⁷ Mama, wa pili kutoka kwako, Bibi Dillman pale. Kama unaamini ya kwamba Mungu atakuponya ugonjwa huo wa tumbo. Bibi Dillman, amini, nawe utaninii tumbo lako. Ni tumbo lenye wasiwasi. Umekuwa nalo kwa muda mrefu, hasa sana tangu ulipokoma hedhi imekusumbua sana. Umekuwa na mambo mengi ya kukusumbua, bali yote yamekwisha sasa. Endapo mambo hayo ni ya kweli, wapungie tu watu mkono wako, kusudi wapate kuona. Kama mimi ni mgeni kwako, endelea kuupunga mkono wako. Yesu Kristo akuponya.

²⁰⁸ Je! mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ni kitu gani? Yehova-Yire, Bwana hujipatia Mwenyewe Dhabihu! Sasa wasikilizaji wote wanakuwa kama ukungu kwangu. Yehova-Yire ametoa dhabihu kwa ajili ya kila mmoja wenu. Mnaamini hivyo?

²⁰⁹ Sasa ninyi hapa mlioinua mkono wenu, njoni hapa na msimame hapa kwa dakika moja. Mtakuja? Yehova-Yire amejiipatia dhabihu. Uliinua mkono wako, ya kwamba uliamini hilo. Mmeona hapa, na mnajua. Haiwezekani. . . Ni Kitu fulani! Waangalieni watu hawa, ni wangapi wameitwa. Sijui sasa. Labda saba, wanane ama kumi, wowote wale waliokuwa, ambao wameitwa. Ingezidi kuendelea tu. Lakini wakati nikiwa na nguvu, ninawatakeni mje, mumkubali Kristo kama Mwokozi wenu. Mwaweza kusimama sasa na mje, wakati tukiimba, “Ninakuja, Bwana, ninakuja Kwako sasa”? Mwaweza kusimama sasa na mje hapa, ninyi mlioinua mkono wenu muda kidogo uliopita? Na msimame kuizunguka madhabahu hapa, na mwonyeshe ya kwamba hammwonei Kristo aibu. Mko Mbele Zake. Njoni sasa, na mwathibitishie watu ya kwamba kweli mlimaanisha jambo hilo, ya kwamba mnataka kukumbukwa na Mungu, na mmemkubali Yeye kama Mwokozi wenu. Njoni huku juu sasa, wakati sote tukisimama na kuimba.

Ninakuja, Bwana!

Ninakuja sasa Kwako!

Nioshe, nisafishe katika ile Damu

Iliyomwagika kutoka Kalvari!

²¹⁰ Ondokeni mje sasa, shukeni mje hapa chini. Tutaomba. Kamwe hutakuwa karibu na Yeye zaidi utakapoondoka.

Ninakuja sasa Kwako!

Nioshe, nisafishe!

²¹¹ Shukeni mje moja kwa moja kutoka kwenye roshani. Hiyo ni kweli. Shukeni moja kwa moja, msimame papa hapa. Iweni ninii. . . Sasa, Yeye alisema, “Kama mtanikiri mbele za watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu. Lakini kama

ukinionea aibu, Mimi nitakuonea aibu,” kumbukeni, Biblia, kutoka Mwanzo hadi Ufunuo. Njoni sasa, vijana kwa wazee. Mtakuja? Mfuasi wa Kanisa, ama si mfuasi, njoo sasa. Je! mtakuja? Mkubali Kristo wakati ukiwa Mbele Zake.

Ninakuja, Bwana!

Ninakuja sasa Kwako!

Nioshe, nisafishe katika ile Damu

Iliyotiririka kutoka Kalvari!

²¹² Endeleeni tu, kuimba. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha, “Ninakuja, Bwana.”—Mh.]

²¹³ Sikilizeni. Je! mnaniamini mimi kwamba ni nabii Wake? Sijapata kukiri jambo hilo hapo kabla. Ninaamini ninasimama na watu wanaofahamu na kujua yale ninayotaribu kuwaelezea. Wapo watu hapa ndani wanaokiri Ukristo, wanapaswa kuwa papa *hapa*. Njoni, je! mtakuja? Hebu niwaulizeni, mtawezaje kupata kuja? Kamwe hamtapokea ishara nyingine. Hii ndiyo Yenyewe. BWANA ASEMA HIVI. Je! nabii wa Mungu angetoa tamshi kama hilo kama halikuwa ni kweli? Mnaipokea ishara yenu iliyo kuu sana, na ndiyo ishara yenu ya mwisho, kabla ya kuonekana kwa Kristo. Njoni! Sababu ya mimi kusema mambo haya, sijapata kusema jambo hili kwenye mkutano mwingine wowote, ninajisikia ya kwamba papa hapa ipo nafasi hapa ya jambo fulani kutukia. Hiyo ndiyo sababu ninasema jinsi ninavyosema. Ninaamini mnafahamu. Msingezunguka-zunguka, muunde namna fulani ya dhehebu, msemi, “Ndugu Branham ni mungu,” ama kitu kama hicho. Mnafahamu yale ninayonena habari zake. Njoni sasa. Njoni. Hebu niwashawishi, katika Jina la Kristo. Njoni!

²¹⁴ Wewe usiyejua mahali unaposimama, huna hakika na jambo hilo, ni wa kiakili tu, ama namna fulani ya mhemuko; umelia, umeomboleza, ama—ama ulikuwa na namna fulani ya mhemuko. Kamwe usijaribu kwenda Kule na hayo. Kumbuka, ninakwambia katika Jina la Bwana, ya kwamba umepotea, umepotea vibaya sana, wala hujui. Usibahatishe, ewe rafiki. Ninapanda tu mbegu, na kulivuta jarife. Mungu anachukua chumo. Sijui.

²¹⁵ Na tuviinamisha vichwa vyetu, tuone kama Yeye hataniambia. [Dada fulani ananena kwa lugha, kisha anafasiri—Mh.] Mnasikia jambo hilo.

Ninakuja sasa Kwako! (Chunguza moyo wako mwenyewe)

Nioshe, nisafishe katika ile . . .

²¹⁶ Mfuasi wa kanisa. Kama nilikuwa nimesimama pale, na nilikuwa tu na tukio la kujiunga na kanisa . . . ? . . . ningekuja hapa upesi tu niwezavyo.

²¹⁷ Kumbukeni, Roho anashuhudia ya kwamba tuko mwisho. Sayansi ilisema, “Ni usiku wa manane kasoro dakika tatu.”

Ujumbe na Biblia husema, “Hili hapa, jambo la mwisho!” Uamsho unaisha. Mlango unafungwa. Utakuwa nje, ukibisha, wala huwezi kuingia. Njoo!

Mungu akubariki, msichana. Sasa, mliona jambo hilo?

Ninakuja, Bwana!

Ninakuja sasa . . .

²¹⁸ Mungu akubariki. Hilo ni sawa, bwana. Hivyo ndivyo inavyopaswa, shuka uje moja kwa moja kutoka kwenye roshani. Njoni kwa safu.

²¹⁹ Hili hapa Neno, huu hapa ushuhuda. Hiyo hapo Roho, huyo hapo shahidi. Na hapa watu wanakuja, kuonyesha ya kwamba tuko hapa kwenye wakati wa mwisho.

Ninakuja, Bwana!

Ninakuja sasa Kwako!

Nioshe, nisafishe katika ile Damu

Inayotiririka kutoka Kalvari.

Ninakuja, Bwana!

²²⁰ Ninangojea, nikiwaita wengine waingie. “Hataki yeyote aangamie; bali wote waifikie ile toba.” “Njoni,” kasema, “Kwangu Mimi.”

²²¹ Kama umekuwa na tashwishi moyoni mwako. Inawapasa kuwa na uhakika, enyi marafiki. Imani ni kamilifu.

. . .kutoka Kalvari!

. . .Bwana!

Ninakuja sasa ku . . .

²²² Kadiri, watu hamsini hadi sabini na tano wamekusanyika hapa. Sasa njoni. Hebu wengine wanaopaswa kuja. Ninashikilia tu kidogo zaidi sasa. Maana, kesho itakuwa ni uponyaji wa Kiungu. Roho Mtakatifu alinena nami, muda mfupi uliopita, “Usifanyize mstari huo. Fanya wito wa madhabahuni.” Nitamtii na kufanya anavyoniambia. Ninajua vema kuliko kutotimiza hilo.

Ninakuja sasa Kwako!

Nioshe, nisafishe katika ile Damu

Iliyotiririka kutoka Kalvari.

Huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa, tuingojea.

²²³ Ee Mungu, jalia Roho Mtakatifu atende kazi katika hawa. Wale wanaotaka kuja mbele madhabahuni, kuwaongoza watu sasa kwenye baraka. Na—na Bwana Mungu na alijalie. Roho wa Mungu, akinena.

²²⁴ Jongeeni ndani, jongeeni ndani. Njoni karibu sasa, kila mmoja. “Kila nafsi, iliyoteswa na dhambi, kuna rehema kwa Bwana.” Njoni sasa. “Wakija chini ya mafuriko yanayosafisha, hupoteza madoa yao yote ya hatia. Kuna Chemchemi iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye vena za Imanueli.” Kwa uchaji.

225 Mnaihisi hiyo amani juu ya mkutano sasa? Ni kitu gani? Ni mauti, mauti kwa wenye dhambi. Sasa wafanyakazi wa kibinafsi wawaendee sasa. Ni mauti, watu hawa wanakufa. Biblia ziko nje, wanaeleza. Mauti inaendelea madhabahuni, na Uzima mpya utakuja baada ya mauti.

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye...

Loo, jinsi utakavyotaka kusikia jambo hilo siku moja, ile siku ambapo kupigapiga kwa moyo wako kutakapokoma kupiga!

Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya
mafuriko hayo,
Wanapoteza madoa yao yote ya hatia.
Wanapoteza madoa yao yote ya hatia,

Jambo ndilo hilo, ewe jamaa mdogo. Nakutakia heri. Hilo ndilo Yeye alikuwa akingojea.

Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya
mafuriko hayo,
Wanapoteza madoa yao yote ya hatia.

226 Sasa hebu Wakristo waliofunzwa, waje wakati tukiimba kifungu kinachofuata. "Yule mwizi aliyekuwa akifa alifurahia kuona ile Chemchemi katika siku yake; hapo naomba mimi, ingawa ni mchafu kama alivyo, nioshwe dhambi zangu zote." Hebu watu watakaowaongoza wasogee karibu sasa. Ninyi ambao hamjapata ubatizo wa Roho Mtakatifu, jongeeni karibu sasa. Hamjui yale Mungu angeweza kufanya sasa katika dakika moja. Jongeeni huku sasa, tunapoimba kifungu kinachofuata sasa.

Yule mwizi aliyekuwa akifa alifurahia...
(Neno lililofanyika mwili)
Chemchemi katika siku yake;

Loo, hilo ni sawa, tokeni moja kwa moja sasa. Njoni wakati yale Maji yanatibuliwa.

...mimi, ingawa ni mchafu kama yeye,
Nioshwe dhambi zangu zote.
Nioshwe dhambi zangu zote,
Nioshwe dhambi zangu zote;

227 Ndiyo hiyo, wafanyakazi. Ingieni mumu humu. Hao wote sasa na waje kwa ajili ya kutibua Maji. Njoni huku.

...mchafu kama yeye,
Nioshwe dhambi zangu zote.

228 Sasa ninyi mnaotaka kuomba, jongeeni karibu sasa na mwe tayari. Tutaamini ya kwamba Mungu ataninii, atatambua jambo hili. Hana budi kulitambua! Mungu yeye yule anayeweza kulitambua wazo la moyo! Kumbukeni, Yesu alifanya jambo hilo

mara moja tu katika mji fulani. Bali Yeye alisema, “Zaidi ya hizi ninyi, mtazifanya.” Unaona, alithibitisha Maandiko Yake kuwa kweli! Jongeeni sasa. Hebu sote tuwaombee watu hawa walio hapa sasa. Kila mtu anayejua jinsi ya kuomba. Ni Wakristo wangapi waliozaliwa mara ya pili walio humu jengoni? Inua mkono wako. Sasa hebu kila mtu tuinue mikono yetu na kutoa shukrani kwa ajili ya watu hawa.

²²⁹ Baba yetu wa Mbinguni, tunatoa shukrani Kwako kwa ajili ya watu hawa. Wao ni Wako. Wanakuja, kuungama. Wanakuja wapate kufa kwa nafsi yao na kwa dhambi. Wanarudi, viumbe vipya katika Kristo.

²³⁰ Shetani, umeshindwa vita! Mungu ni Yehova-Yire! Bwana amejipatia Dhabihu, amejipatia watu fulani, akatoa wito wa madhabahuni, akatoa Ujumbe, akatoa neema. Na Shetani ameshindwa vita, katika Jina la Yesu Kristo ameshindwa vita!



YEHova-YIRE ³ SWA62-0707
(Jehovah-Jireh ³)

MFULULIZO WA YEHova-YIRE

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marriion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, tarehe 7 Julai, 1962, katika Ukumbi wa Manispaa huko Grass Valley, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org